

**KLABU ANAZOWEZA KWENDA VAN DIJK**
UKURASA 11

**SABABU** mpya vyura Kihansi kutorejeshwa eneo la asili
UKURASA 8

**AKAUNTI** ya NMB bila makato ya mwezi yapokewa kwa shangwe
UKURASA 8



**WALIMU** matatani kutoza michango ya madawati
UKURASA 16


# Nipashe

Jumatatu Februari 12, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581584

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguard


# UPEKEE WA LOWASSA





**VIGOGO** pande zote waibuka na kauli za kushtua; Rais Samia kuongoza maziko Monduli... *Endelea ukurasa* 2 & 3



DK. Amani Karume



Prof. Anna Tibaijuka



Freeman Mbowe



Dk. Harrison Mwakyembe



Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, akitia saini kitabu cha maombolezo cha aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa, nyumbani kwake Masaki, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Samia atua Vatican kuteta na Papa

**AAMBATANA** na kikosi cha Katoliki Tanzania... *Ukurasa 3*

## Gekul aitwa Korti Kuu rufani madai ya udhalilishaji

UKURASA 19

**MICHEZO** **YANGA SC KILELENI RAUNDI YA KWANZA** UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa na mkewe Mbonimpaye Mpango wakiwapongeza Askofu Dk. Abel Godson Mollel na msaidizi wake Mchungaji Lareiton Lukumay baada ya kuwekwa wakfu na kuingizwa kazini katika ibada iliyofanyika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Kati Usharika wa Kimandolu mkoani Arusha jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Vigogo waibua upekee wa Lowassa

**Na Waandishi Wetu**

NCHI inaomboleza kifo cha Waziri Mkuu wa zamani, Edward Lowassa (70), huku wanasiasa wakiibua mambo mbalimbali yanayoonesha upekee wake kisiasa na kiuongozi.

Lowassa aliweka historia ya kuwa kiongozi wa kwanza wa wadhifa huo kujiuzulu mbele ya Bunge, kuhamia upinzani na kugombea urais huku akiwa ni mwanasiasa mwenye nguvu na aliyetikisa katika kila nyadhifa alizoshika.

Jana viongozi na wananchi walimiminika nyumbani kwa Lowassa, Masaki jijini Dar es Salaam kuifariji familia huku wakimwelezea kama kiongozi shupavu, aliyesimamia alichokiamini na mwenye kufanya uamuzi mgumu pasi na kuogopa huku akitanguliza mbele maslahi ya nchi.

Lowassa anatajwa kuwa kiongozi aliyekuwa na nguvu ya ushawishi ndani na nje ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na hata alipokatwa kugombea nafasi ya urais mwaka 2015, alihamia CHADEMA na baada ya matokeo ya urais kutangazwa, wafuasi wake walitaka kuingia mtaani lakini aliwatuliza na kusema kuwa hataki urais wa utokanao na kumwaga damu za watu.

Katika mitandao ya kijamii zimesambazwa picha za 'mafuriko yake' ya watu wakati akirudisha fomu ya kugombea urais kwa tiketi ya CHADEMA kwenye ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Posta, jijini Dar es Salaam pamoja na mikutano ya hadhara katika majiji ya Mbeya, Dar es Salaam, Arusha iliyochagizwa na kaulimbiu ya "Mabadiliko Lowassa! Lowassa Mabadiliko!"

**KUZIKWA JUMAMOSI**

Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuongoza mazishi ya mwili wa Lowassa yatakayofanyika Februari 17, mwaka huu katika Kijiji cha Ngarash, wilayani Monduli, mkoani Arusha.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alibainisha hayo jana alipotoa salamu za pole kwa familia ya marehemu nyumbani kwa Lowassa, Masaki, jijini.

"Watanzania pamoja na wanafamilia tutaongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuupeleka mwili kwenye nyumba ya milele," alisema Waziri Mkuu.

Alisema ratiba ya safari hiyo itaanzia kesho ambapo mwili wa marehemu utafanyiwa ibada fupi na kuagwa na wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam katika Viwanja vya Karimjee kuanzia saa 2:50 asubuhi mpaka saa saba mchana kisha utarudishwa Hospitali ya Jeshi Lugalo.

Alisema kuwa Jumatano mwili utatolewa nyumbani hadi Kanisa la KKKT Azania Front kwa ajili ya misa takatifu inayotarajiwa kuanza saa nne asubuhi hadi saa saba mchana na waombolezaji watakaokuwapo kanisani watapata nafasi ya kuaga mwili.

Alisema kuwa Alhamisi mwili utasafirishwa kwenda Arusha kwa kutumia ndege. Watatua Uwanja wa Ndege Arusha au Kilimanjaro (KIA). Maelekezo kuhusu hili yatatolewa baadaye na wanatarajiwa kufika Monduli saa nane mchana.

Alisema kuwa Ijumaa, wananchi wa Monduli wataaga mwili wa aliyekuwa mbunge wao (1990-2015).

Lowassa aliwahi kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais (Haki na Mambo ya Bunge), Waziri wa Ardhi na Makazi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Kuondoa Umaskini), Waziri wa Maji na Mifugo na mwaka 2005 aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu.

**FREEMAN MBOWE**

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, ametuma salamu za pole kwa familia na kueleza kuwa taifa litamkumbuka Lowassa kwa mambo mengi kwa kuwa alikuwa mstari wa mbele kupigania mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi.

Mbowe alisema amepokea kwa mshtuko na majonzi taarifa za kifo cha Lowassa, amempoteza rafiki, ndugu na mshauri mzuri.

"Tanzania na dunia imepoteza kiongozi shujaa, mwenye mchango mkubwa katika kujenga amani, ushirikiano na ustawi wa jamii.

"Alikuwa kiongozi shupavu, mwanasiasa mahiri, mwanaharakati hodari na alikuwa mstari wa mbele kupigania mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi nchini mwetu," alisema Mbowe akimtaja Lowassa alikuwa mtu mwenye hekima, busara, ujasiri, uzalendo, huruma, upendo na msamaha kwa wote, mtu mwenye maono, mipango na mtekelezaji mzuri wa miradi ya maendeleo kwa manufaa ya wananchi.

"Tutaendelea kuenzi kazi, mawazo na hekima alizotuachia Mheshimiwa Lowassa. Tutaendelea kumwombea na kumkumbuka kwa mema aliyotutendea," alisema Mbowe.

**JAJI WARIOBA**

Viongozi waliofika nyumbani kwake jana ni pamoja na Waziri Mkuu mstaafu Jaji Joseph Warioba, aliyesema taifa limepoteza kiongozi mwenye upendo, utu na aliyepinga kuoneana kwenye siasa.

Alisema alimfahamu Lowassa kama kiongozi mwenye msimamo na asiyekata tamaa, aliyeamini katika elimu na ajira kwa vijana na hata alipokuwa Waziri Mkuu, alianzisha shule za sekondari za kata ili kuboresha upatikanaji elimu na kuwezesha watoto wa kitanzania kuendelea na masomo.

Kwa mujibu wa Warioba, wakati wa uongozi wake, Lowassa alikuwa mfuatiliaji mzuri wa utekelezaji wa yale yaliyoazimiwa na serikali.

"Pamoja na matatizo, Lowassa hakutetereka, aliendelea kuwa kiongozi, alikuwa na maono na imani yake," alisema.

**NAZIRI KARAMAGI**

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kagera, Naziri Karamagi, alisema Lowassa alikuwa akipinga kuoneana katika siasa, alisisitiza wanasiasa wawe kitu kimoja na kufuata utaratibu waliojiwekea, hali iliyosababisha mwaka 2015 wapinzani kupata viti vingi.

Alisema pia alibadilisha dhana ya kilimo kwanza kuwa elimu kwanza, akiamini kuwa bila elimu hakuna kilimo, hali iliyochangia kuwa na wakulima wasomi.

Alisema yeye ni mmoja wa watu walioshawishiwa na kiongozi huyo kuingia kwenye siasa mwaka 2003 na tangu wakati huo alikuwa naye bega kwa bega akimwongoza na kumpa ushauri.

"Ukianguka ataanguka na wewe, ukisimama atasimama na wewe, hivyo ndivyo alivyokuwa Lowassa na ndio maana watu wengi walikuwa wanampenda," alisema.

**BALOZI ADADI**

Aliyekuwa Balozi wa Tanzania Zimbabwe na Mbunge wa Muheza, Adadi Rajabu alisema Lowassa alipenda maendeleo ya watu na hakupenda kuona wananchi wanaishi maisha ya shida.

Balozi Adadi ambaye alikuwa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), alitolea mfano kuwa alikwenda Misri kujenga hoja ili wananchi wa mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora na mengineyo wapate maji yanayotoka Ziwa Victoria na alifanikiwa na sasa wananufaika.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, alisema anamkumbuka mwanasiasa huyo wa utu wake na wakati wa uongozi wake alitumikia wananchi kwa moyo mmoja. Alijifunza kwake uzalendo na kuipenda nchi kwanza.

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Goodluck Ole-Medeye, alisema Lowassa alikuwa anapenda

Inaendelea Uk.3

HABARI KITAIFA

# Samia atua Vatican kuteta na Papa

## •Aambatana na kikosi cha Katoliki Tz

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameambatana na viongozi watano wa vyama vya kitume vya Kanisa Katoliki Tanzania kwenda kumwona Kiongozi wa Kanisa hilo duniani, Papa Francis, huko Vatican, Roma.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Rais Samia atakutana na Papa Francis kwenye ofisi za Papa na kufanya mazungumzo ya faragha.

Wizara hiyo imeeleza kuwa baada ya mazungumzo hayo, Papa atakutana na ujumbe mzima wa Rais Samia ambao unajumuisha Mwenyekiti wa Halmashauri ya Walei Wakatoliki Tanzania, Prof. Deogratias Rutarora na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Walei-Zanzibar, Dalmas Gregory.

Wengine katika ujumbe huo ni Mwenyekiti wa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) na Rais wa Wanawake Wakatoliki Afrika, Evaline Ntenga, Mwenyekiti wa Utoto Mtakatifu Jimbo la Dar es Salaam, Theresia Sedan na Mwenyekiti wa Vijana Wakatoliki Wafanyakazi Tanzania, Leonard Mapolu.

Kiongozi huyo akiwa nchini humo baada ya kukutana na Papa Francis, atakutana na Kardinali Pietro Parolin, Msaidizi Mkuu wa Papa, Paul Gallagher, Waziri wa Uhusiano wa Kimataifa wa Vatican.

Tanzania na Vatican tangu mwaka wa 1960 zimekuwa zikishirikiana katika masuala ya elimu, afya, amani na kiroho.

"Kanisa Katoliki linakadiriwa kumiliki zaidi ya shule za chekechea 240, shule za msingi 147, shule za sekondari 245, vyuo vya ufundi 110, vyuo vikuu vitano na linaendesha taasisi za afya 473 nchini," ilibainishwa katika taarifa hiyo wizara.

Tofauti za udini hazijawafanya viongozi hao kushindwa kukaa pamoja na kujadili maslahi ya wananchi na uendelezaji ushirikiano kati ya nchi hizo mbili.



# Vigogo waibua upekee wa Lowassa

**Inatoka Uk. 2**

watu wote na hakukubali kuona yeye ameshiba ilhali mtu mwingine ana njaa, alikuwa kiongozi mnyenyekevu na asiyependa majungu.

"Alikuwa mbunifu na mwenye mawazo mapana, hata siku moja huwezi kumkuta akimteta mtu, alitaka ukienda kwake uende na mawazo au mapendekezo ya maendeleo," alisema.

**ACT WAZALENDO**

Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha ACT- Wazalendo, Juma Haji, alisema kuwa wakati wa uhai wake, Lowassa alikuwa kiongozi aliyetumikia nchi kwa moyo mkunjufu katika nafasi mbalimbali alizoshika.

Duni alisema chama chao kimetangaza bendera zake zitapepea nusu mlingoti kwa siku tano za maombolezo zilizotangazwa na Rais Samia.

**RAIS KARUME**

Rais mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Amani Abeid Karume alisema Lowassa alikuwa mchapakazi, mwenye uthubutu katika kufanya uamuzi na maisha yake ya siasa kwa ujumla.

Rais huyo mstaafu alisema taifa limepoteza mtu ambaye alikuwa shupavu katika siasa za Tanzania na "hodari sana".

Karume alisema akiwa Rais, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar waliendelea kushirikiana zaidi na Lowassa ambaye wakati huo alikuwa Waziri Mkuu wa Tanzania.

"Tulipokuwa bungeni tunapitisha muswada kuruhusu mfumo wa vyama vingi, ninakumbuka wale wenzangu na mimi tulikuwa kundi moja tulikuwa tunaunga mkono muswada ule, kwa sababu tuliona ungepeleka nchi yetu mbele zaidi na Lowassa alikuwa mmoja wa 'machampioni' kwa demokrasia ya nchi yetu hii," alisema Karume.

Kuhusu kujiuzulu kwa Lowassa katika nafasi ya Waziri Mkuu, Karume alisema hilo ni jambo la kawaida kisiasa na kwa wanasiasa kama ajali ya kisiasa na kwamba yeye (Karume) halikumshtua.

**PROF. TIBAIJUKA**

Aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Prof. Anna Tibaijuka aliandika katika ukurasa wake wa X; "Familia ya Lowassa poleni. Taifa twaomboleza kifo cha kjiongozi 'STATESMAN'. Nilishuhudia ukiweka maslahi ya nchi mbele ya yako.

"Jina lilipokatwa nilikushauri ubaki CCM kimfumo uwezekano kutangazwa mshindi ukitokea upinzani HAUPO, ukanijibu 'NAJUA ila hutaki Manyanyaso kuendelea'. R.I.P."

**SWAHIBA MGEJA**

Khamisi Mgeja, aliyekuwa Mwenyekiti CCM Mkoa wa Shinyanga na kuamua kuacha wadhifa wake akimfuata swahiba wake wakati huo Lowassa anahamia CHADEMA, alisema jana kuwa kiongozi huyo alikuwa mtu mwenye uthubutu kiutendaji.

"Haikujalisha kwa kipindi hicho tulikuwa wengi tulioamua kujitoa mwanga bila kujali maslahi ya nafasi zetu kwa kauli moja kwani tuliamini kuwa kiongozi huyo alikuwa na uwezo mkubwa wa kiutendaji na pia alikuwa na uthubutu katika kuwatetea wananchi pamoja na taifa kwa ujumla," alisema Mgeja.

Agosti 13, 2015 Mgeja alitangaza kujiuzulu nafasi zake ndani ya CCM na kuhamia CHADEMA kwa kauli waliyoitumia kuwa "CCM si baba yangu, siyo mama yangu, Watanzania wanahitaji mabadiliko".

"Hata alipokuwa CHADEMA hakutaka vurugu wala kuona damu za Watanzania zinamwagika kisa yeye, hivyo alizuia maandamano yaliyotakiwa kufanya na vijana licha ya kujua kuwa alikuwa ameshinda uchaguzi huo na kwa hilo tu kila mwanasiasa anayewatetea wananchi hawezi kuacha kuenzi maisha ya Lowassa," alisisitiza Mgeja.

**SWAHIBA MSINDAI**

Mwenyekiti mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, Mgana Msindai, alisema taifa limempoteza kiongozi mahiri aliyekuwa mtawala wa kutukuka, asiyeogopa na alifanya uamuzi wa mambo ya maendeleo na kuyasimamia hadi yakaleta matokeo chanya.

Msindai alisema Lowassa atakumbukwa kwa mengi aliyoyafanya wakati wa uhai wake, lakini kubwa zaidi ni kuanzisha shule za sekondari za kata ambazo kwa sasa zinatawala na zimeanza kufaulisha vizuri.

Mkuu wa Mkoa wa Singida ambaye alikuwa swahiba wa Lowassa, Peter Serukamba, alisema amepokea kwa masikitiko kifo cha Lowassa na taifa limepoteza mmoja wa wazalendo wake.

**HARRISON MWAKYEMBE**

Waziri mstaafu katika wizara mbalimbali, Dk. Harison Mwakyembe alisema amepokea taarifa ya kifo cha Lowassa kwa masikitiko makubwa kwa kuwa Watanzania akiwamo yeye (Dk.Mwakyembe) walikuwa wanahitaji mchango wake wa mawazo.

"Hili halina ubishi kwamba Lowassa alikuwa hazina kubwa ya mawazo na ushauri chanya katika ujenzi wa taifa letu.

"Nitumie nafasi hii kuitakia familia ya marehemu na Watanzania wote wakiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu cha majonzi na maombolezi," alisema.

**ALBERT CHALAMILA**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema Lowassa aliwafundisha namna kiongozi anapaswa kuwa na uvumilivu wa kisiasa katika uongozi.

Alisema kiongozi huyo alikuwa ni mwalimu na daraja la usuluhishi katika siasa na mara zote alionesha kuwa siasa si uhasama kwa kuwa nia ni moja - kutumikia wananchi.

**PAUL MAKONDA**

Jana Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, alitangaza kusitisha ziara yake ya mikoa 19 ambayo ilibaki ya Mtwara na Lindi ili kuomboleza kifo cha Lowassa.

"Kwa mashauriano na hekimu kubwa iliyotuongoza tumeona ni vyema kuahirisha ziara ili tuungane na Watanzania wote katika kipindi hiki cha maombolezo na sisi CCM ambacho amekitumikia tangu akiwa kijana ameshika nafasi nyingi, tuwaombe wananchi katika mikoa iliyobaki ya Mtwara na Lindi ziara yetu tutaipanga tena," alisema Makonda.

Juzi alasiri, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alitangaza kifo cha Lowassa na kubainisha kuwa Rais Samia ametangaza siku tano za maombolezo kitaifa kuanzia juzi.

***Imeandaliwa na Jenipher Gilla, Elizabeth Zaya, Beatrice Shayo (DAR), Thobias Mwanakatwe (SINGIDA) na Vitus Audax (MWANZA)**


**WAFANYA BIASHARA WA MAKAA YA MAWE/WAUZAJI WA MAKAA YA MAWE WANAKARIBISHWA**

Kampuni ya kimataifa inayojihusisha na uchimbaji wa madini Mikoa ya mbeya na songea,inatafauta na kuhitaji mfanyabiashara au wafanyabishara wa NDANI na WAKIMATAIFA katika kuuza bidhaa yake ya MAKAA YA MAWE

Kwa unyenyekevu mkubwa unaweza kushiriki au kueleza mawazo yako katika namna unavyojihusisha au kama unapenda kujishughulisha na kazi hii na kutoa taarifa za kina za udhoefu wako katika uuzaji wa makaa ya mawe ndani ya siku saba(7)kwa kutuma taarifa yako kwenye nukushi ifuatayo

**coaltanzania@gmail.com**

# Bandari ya Mtwara yapata mtambo unaoshusha makontena 25 kwa saa

**Na Joseph Mwendapole,**
MTWARA

BANDARI ya Mtwara ambayo ina uwezo wa kuhudumia tani milioni moja za shehena kwa mwaka, imepata mtambo wa kisasa uitwao Ship to Shore Gantry Crane (SSG), wenye uwezo wa kuhudumia makontena 25 kwa saa.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Meneja wa Bandari hiyo, Ferdinand Nyathi, wakati akiwaeleza wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari kuhusu maboresho yanayofanyika kwenye bandari hiyo.

Alisema mtambo huo wa SSG tayari umeshasimikwa na kuongeza kuwa mbali na hiyo pia wamepata scanner moja yenye uwezo wa kuhudumia makontena 30 kwa saa.

Alisema hayo imetokana na maboresho makubwa yaliyofanywa kwenye bandari hiyo yakihusisha pia ujenzi wa gati moja la nyongeza lenye kina cha mita 13 na urefu wa mita 300.

Nyathi alisema Bandari ya Mtwara inarahisisha shughuli za biashara kwa mikoa ya kusini mwa Tanzania na Zanzibar pamoja na nchi za Msumbiji, Comoro, India na Vietnam.

Alisema bidhaa kuu zinazopita Bandari ya Mtwara ni pamoja na korosho ghafi, saruji, bidhaa za chakula, shehena za miradi, mafuta, makaa ya mawe na mizigo mchanganyiko.

"Mbali na ufanisi ambao mteja anaupata akipitisha mzigo kwenye Bandari ya Mtwara pia anapata faida ya asilimia 30 ya unafuu wa tozo tofauti na angepitisha kwenye bandari zingine," alisema.

Kiongozi huyo alibainisha kuwa mwaka 2018/219, Bandari ya Mtwara ilihudumia meli 141, mwaka 2019/20 meli 110, 2020/21 meli 84, 2021/22 meli 166 2022/23 meli 313 na Julai 2023 mpaka Januari 2024 meli 187.

Alisema Bandari ya Mtwara ina maghala mawili ya kuhifadhi mizigo yenye ukubwa wa mita za mraba 12,500 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 18,000 za shehena kwa wakati mmoja.

Alitaja fursa zilizoKo mkoani Mtwara kuwa ni shughuli za utafutaji mafuta na gesi, uzalishaji gesi asilia na bidhaa zitokanazo na gesi.

Alitaja fursa nyingine kuwa ni kuwapo bidhaa za madini na viwanda mbalimbali katika Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara (Mtwara Development Corridor) na nchi jirani za Malawi, Msumbiji na Zambia.

Alitaja changamoto zinazoikabili Bandari ya Mtwara kuwa pamoja na ukosefu wa miundombinu ya usafirishaji ardhini kama reli ambayo ingekuwa kiunganishi kutoka maeneo ya uzalishaji kama migodi ya Mbamba Bay, Mchuchuma na Liganga.

Alisema pia kuna ukosefu wa meli za mwambao za uhakika ambazo zingesaidia kusafirisha bidhaa mbalimbali kutoka Mtwara kwenda Tanga na kutoka Dar es Salaam kwenda Comoro.

Nyathi alisema Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) imedhamiria kuboresha utendaji wa Bandari ya Mtwara ili itoe huduma kwa nchi jirani za Comoro, Malawi, Msumbiji na Zambia.

Alisema maboresho hyo yatasaidia kutoa huduma pia mikoa ya ukanda wa kusini mwa Tanzania kama Lindi, Mtwara na Ruvuma ili kunufaika na fursa kubwa za kiuchumi zilizopo.

"Rai yetu ni kuiomba serikali kuendelea kutekeleza mipango yake katika kuboresha miundombinu ya usafirishaji nchi kavu hasa reli, ili kuchochea matumizi ya Bandari ya Mtwara kwa kuiunganisha na maeneo mbalimbali," alisema Nyathi.

# OUT yajivunia kuimarisha huduma kwa wanafunzi

**Na Dk. Mohamed Maguo**

CHUO Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kinajivunia kuimarisha huduma kwa wanachuo wake ambao karibu asilimia 95 ni watu wenye majukumu ya kazi na shughuli za biashara, kilimo na ufugaji, uvuvi, machinga, mamalishe na babalishe.

Tangu OUT ilipoanzishwa mwaka 1992 na kuanza kutoa mafunzo mwaka 1994, kumekuwa na kuimarika kwa hali ya juu katika kutoa huduma kwa wanafunzi wa ngazi mbalimbali za masomo.

Hayo yalisemwa na Prof. Deus Ngaruko ambaye ni Naibu Makamu wa OUT anayesimamia Taaluma, Utafiti na Huduma za Ushauri wa Kitaalamu wakati akifunga warsha ya mafunzo ya uandishi wa matini za kufundishia na kujifunzia kwa wahadhiri wa OUT iliyofanyika jijini Dodoma kwenye kituo cha OUT kuanzia tarehe 6 hadi 9 ya mwezi huu.

Akifunga warsha hiyo, kiongozi huyo alisema, "OUT imepiga hatua kubwa sana katika kuimarisha huduma kwa wanachuo na kazi ya mafunzo mliyokuwa nayo kwa siku nne hapa Dodoma ni sehemu ya kuhakikisha huduma kwa wanafunzi zinazidi kuimarika.

"Chuo kilipoanzishwa mwaka 1992 na kuanza kufundisha mwaka 1994 kimeweza kuwa na matini za kujifunzia na kufundishia za aina mbalimbali. Tulianza kwa kutumia matini kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi, Chuo Kikuu Huria cha Nigeria, Chuo Kikuu cha Afrika ya Kusini na sehemu nyingine.

"Mwanzoni mwa miaka ya 2000 tuliandika matini zetu wenyewe kwa kutumia wataalamu wa OUT na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Matini hizo zipo na zinawasaidia sana wanafunzi kujisomea wakiwa mahali popote pale wakiendelea na shughuli zao bila kuziacha," alisema Prof. Ngaruko.

Fauka ya hayo, Prof. Ngaruko aliongeza kwamba, OUT ilipiga hatua nyingine kubwa kwa kuingiza matini za kufundishia na kujifunzia kwenye CD ambapo matini za masomo husika ziliwekwa kwenye CD moja na kusambazwa kwa wanafunzi kupitia vituo vyote vya mikoa na uratibu vya OUT nchi nzima.

Hiyo ilikuwa ni katika kipindi ambapo kompyuta zilianza kuingia nchini. Baadaye katika miaka ya 2007 ukaja mfumo wa Ufundishaji na Ujifunzaji Kielektroniki (MOODLE) ambapo matini za kufundishia na kujifunzia zilianza kupakiwa kwenye mfumo huo na wanafunzi kuweza kujisomea wakiwa wanaendelea na kazi na shughuli zao huko huko waliko.

Kufuatia maendeleo yote haya, Prof. Ngaruko alipongeza Kurugenzi ya Machapisho, Utafiti na Uvumbuzi kwa kazi nzuri ya kuandaa mafunzo haya kwa wahadhiri na kutaka yawe ni mafunzo endelevu kwa wahadhiri wote wa OUT.

Matini zitakazozalishwa kutokana na mafunzo haya zitachapishwa katika nakala ngumu na nakala laini, zitapakiwa kwenye mifumo kama ilivyo hivi sasa.

Awali akitoa mrejesho wa namna mafunzo yalivyofanyika kwa muda wa siku nne, Mhadhiri Mwandamizi wa OUT, Dk. Proches Ngatuni alisema mafunzo yaliyotolewa kwa wahadhiri ni nyenzo muhimu kwa walimu na yatawasaidia katika kuandaa matini za kufundishia na kujifunzia zenye ubora wa viwango vya juu.

Prof. Modest Varisanga ambaye ni Rais wa Jumuiya ya Wanazuoni wa OUT na Profesa Mshiriki katika Kitivo cha Sayansi, Teknolojia na Taaluma za Mazingira, alipongeza Menejimenti ya OUT kwa hatua hiyo kubwa ya kutoa mafunzo ya uandishi wa matini za kufundishia na kujifunzia, yamekuja wakati mwafaka.

Prof. Raphael Gwahula ambaye ni Mratibu wa Machapisho katika Kurugenzi ya Machapisho, Utafiti na Uvumbuzi, alidokeza kwamba OUT ina sera nzuri ya uandishi wa matini za kufundishia na kujifunzia ambayo inaeleza hatua mbalimbali za uandishi pamoja na wajibu na motisha kwa walimu watakaoandika matini hizo.

Dk. Harrieth Mtae ambaye ni Mkurugenzi wa Machapisho, Utafiti na Uvumbuzi alishukuru washiriki wote wa warsha hiyo wapatao 27 kutoka idara mbalimbali za kitaaluma za OUT kwa kuwa wazingativu na watulivu katika siku zote za mafunzo.

Pia alishukuru Menejimenti ya OUT kwa ujumla kwa uwezeshaji na pia uongozi wa kituo cha OUT Dodoma, wenyeji wa warsha hiyo kwa mapokezi mazuri katika siku zote za mafunzo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni ya 20 (4) ya Kanuni za Mafuta Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Rejareja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| **Jina la awali la kituo:** | Poly Petroleum Limited |
| **Nambari ya Leseni:** | PRL-2021-063 |
| **Mahali Kituo kilipo:** | Kiwanja Na. 107, Kitalu "A", Eneo la Msongola, Manispaa ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam |
| **Jina linalopendekezwa:** | Suad Noorhussein Mohamed T/A Poly Petro Fuel |
| **Mmiliki wa awali:** | Poly Petroleum Limited |
| **Mmiliki mpya:** | Suad Noorhussein Mohamed T/A Poly Petro Fuel |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe ya tangazo hili.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA**

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

# MWITO WA KUTOA MAONI

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.**

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131(1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni | Aina ya Ombi la Leseni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Sovavi Oil, S.L.P 11702, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 80, Kitalu "A", Orkesumet, Simanjiro, Manyara. | Elinisafi Elinazi Lukenga (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi jipya |
| 2. | Kastuli Filling Station – Mbulu, S.L.P 306, Karatu. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "F", Eneo la Uhuru, Mbulu, Manyara. | Samwel Kastuli Amsi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la kuhuisha leseni |
| 3. | Mariki Enterprises Limited, S.L.P 8915, Moshi. | Shamba Na. 175, Kitalu "A", Eneo la Longuo, Kata ya Longuo "B", Moshi, Kilimanjaro. | Tadei Ansel Mariki (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la kuhuisha leseni |
| 4. | Marwa William Matiku, S.L.P 872, Musoma | Kiwanja Na. 92,93,94,95 & 96, Kitalu "B" Eneo la Mugumu, Serengeti, Mara. | Marwa William Matiku (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 5. | Afroil Investment Limited, S. L. P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1379, Eneo la Bweri, Musoma, Mara. | Hilmy Ahmed (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 6. | Bageni Company Limited, S. L. P 586, Kahama. | Kiwanja Na.1, Kitalu "B", Eneo la Bukoli, Geita. | Manyengo Bageni Nyamrere (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 7. | Bageni Company Limited, S. L. P 586, Kahama. | Kiwanja Na. 28, Kitalu "A", Eneo la Nyakagwe, Geita. | Manyengo Bageni Nyamrere (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 8. | Nyarugusu Filling Station Limited, S. L. P 71, Geita. | Kiwanja Na. 14, Kitalu "K", Eneo la Katoro, Geita. | Yona Kulwa Joseph (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 9. | Nicodemus Henry Maganga, S. L. P 22, Masumbwe. | Eneo la Lulembela, Mbogwe, Geita. | Nicodemus Henry Maganga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 10. | Alinda's Transport & Oil Products Limited, S. L. P 159, Kyerwa. | Kijiji cha Nyamiyaga, Kyerwa, Kagera. | Amos Daudi Kaihura (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 11. | Karagwe Oils Company Limited, S. L. P. 484, Karagwe. | Kiwanja Na. 53, Kitalu "C", Eneo la Omurushaka, | Seleman Zahor Mansoor (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 12. | Narscis Laurent Kabipi T/A Kabipi Filling Station, S. L. P 64, Malya. | Kiwanja Na.15, Kitalu "G", Eneo la Malya, Kwimba, Mwanza. | Narscis Laurent Kabipi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 13. | Canuck Company Limited, S.L.P 472, Shinyanga. | Kiwanja Na. 1, Eneo la Isaka, Kahama, Shinyanga. | Chad David Beattie (Raia wa Afrika Kusini) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi | Ombi la Leseni Mpya |
| 14. | Tazama Pipelines Ltd - Tank Farm, S.L.P 2157, Dar es Salaam. | Eneo la Tungi, Kigamboni, Dar es salaam. | Patrick Mnzava (Mtanzania) | Leseni ya kuhifadhi mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 15. | Sahara Tanzania Limited, S.L.P 76173, Dar es Salaam. | Eneo la Vijibweni, Kigamboni, Dar es salaam. | Diana Kokushaba Matondane (Mtanzania) | Leseni ya kuhifadhi mafuta | Ombi la kuhuisha Leseni |
| 16. | Mogas Tanzania Ltd, S.L.P. 70284, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 310/3, Eneo la Kurasini, Temeke, Dar es | Emmanuel Nkya (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 17. | DMB Petroleum Limited, S.L.P 42445, Dar es Salaam. | Eneo la Kiluvya madukani, Ubungo, Dar es Salaam | Dahir Mbarak Salim. (Mtanzania) | Leseni ya Mafuta ya jumla | Ombi la Leseni Mpya |
| 18. | Admire Oil Limited, S.L.P 7494, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2092, Kitalu "U", Eneo la Mbagala Kizuiani, Ilala, Dar es Salaam. | Said Mire Artan (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 19. | OKPLAST Limited, S.L.P 8812, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 89/90, Eneo la Vingunguti, Ilala, Dar es Salaam. | Fadl Abbas Ghaddar (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya vilainishi | Ombi la Leseni mpya |
| 20. | Ameir Ally Said Binzoo, S.L.P 1571, Dar es Salaam. | Eneo la Magomeni, Kinondoni, Dar es Salaam. | Ameir Ally Said Binzoo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 21. | GBP Tanzania Limted-Ukonga Service Station, S.L.P 3728, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2110, Kitalu "C" Eneo la Ukonga, Ilala, Dar es Salaam. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la kuhuisha Leseni |
| 22. | Clock Tower Gapco Service Station, S.L.P 9103, Dar es Salaam. | Eneo la Clock tower, Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam. | Mamadou Ngom (Raia wa Senegali) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la kuhuisha Leseni |
| 23. | Admire Oil Limited, S.L.P 7494, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 141, Eneo la Misugusugu, Kibaha, Pwani. | Said Mire Artan (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la kuhuisha Leseni |
| 24. | Sultanate Energy Company Limited, S.L.P 23197, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "M" Eneo la Vikindu, Mkuranga, Pwani. | Mbeki Loshilu Millya (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la kuhuisha Leseni |
| 25. | Delvine Transportation and Supply, S.L.P 100246, Dar es Salaam. | Kijiji cha Vianzi, Mkuranga, Pwani. | David Jackson Massam (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 26. | Kobil Nero Service Station, S.L.P 16351, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 92, Kitalu "B", Eneo la Chalinze, Bagamoyo, Pwani. | Yuda Peniel Mosha (Mtanzamia) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la kuhuisha Leseni |
| 27. | Jahida Hassan Saidi T/A Akangene Petrol Station, S.L.P. 200, Dar es Salaam. | Kiwanja Na 24, Kitalu "F", Eneo la Mnazi mmoja, Lindi. | Jahida Hassan Saidi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 28. | Bs Oil (T) Ltd - Nanjilinji Filing Station S.L.P 193, Kilwa | Kijiji cha Nanjilinji, Kilwa, Lindi. | Yusuph Barakat (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la kuhuisha leseni |
| 29. | Acer Petroleum (T) Ltd – Nagaga, S.L.P 78845, Dar es Salaam. | Kijiji cha Nagaga, Masasi, Mtwara. | Atul Mital (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la kuhuisha Leseni |
| 30. | Acer Petroleum (T) Ltd – Napupa, S.L.P. 78845, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 551, Kitalu "A", Eneo la Napupa, Masasi, Mtwara. | Atul Mital (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la kuhuisha Leseni |
| 31. | Tanzania Breweries Limited – Mbeya Brewery Plant, S.L.P 6314, Mbeya. | Kiwanja Na. 16 & 17, Iyunga, Mbeya. | Richmond Raymond (Mtanzaia) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 32. | SBC Tanzania Limited – Mbeya Branch, S.L.P 2635, Mbeya. | Kiwanja Na. 25, Iyunga, Mbeya. | Ziad Anwar El-Khalil (Raia wa Uingereza) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi | Ombi la Leseni Mpya |
| 33. | Frank Fred Mwankenja – Mwankenja Filling Station, S.L.P 45, Tukuyu | Kiwanja Na. 42, Kitalu "A", Kiwira, Rungwe, Mbeya. | Frank Fred Mwankenja (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 34. | Saatatu Investment Limited – Mlowo Filling Station, S.L.P 14, Mbozi | Kiwanja Na. 6, Kitalu "F", Mlowo Mjini, Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe | Yona Saatatu Chaula (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 35. | Acer Petroleum Tanzania Limited, S.L.P 78845, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 284 & 285, Kitalu "P", Mjimwema, Njombe. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 36. | Olympic Petroleum (T) Ltd – Matai, S.L.P 6185, Mwanza. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Matai, Kalambo, Rukwa. | Ally Mohamud Adon (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 37. | Kipunde Filling Station, S.L.P 830, Chemba. | Kijiji cha Tandala, Chemba, Dodoma. | Jam Issa Said Kipunde (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 38. | Juma Waziri Ndiyumviye Petrol Station, S.L.P 3482, Dodoma. | Kijiji cha Mpamatwa, Bahi, Dodoma | Juma Waziri Ndiyumviye (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

## MAONI & UCHAMBUZI

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

## TPLB isifumbie macho kelele hizi kwa waamuzi

KELELE kuhusu uchezeshaji mbaya wa waamuzi zimeanza tena kusikika ligi ikielekea mzunguko wa pili ambao ndio hupatikana bingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara atakayekwenda kuiwakilisha nchini katika Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Labda unaweza ukadhani ni kwa sababu tu ya mechi ya Ijumaa kati ya Simba dhidi ya Azam FC, uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza na kumalizika kwa sare ya bao 1-1, hapana.

Hata makocha sasa wameanza kuwalalamikia waamuzi kuelekea kwenye mzunguko wa pili, tofauti na ule wa kwanza, ambapo kwa kiasi fulani hali ilitulia. Cha kushangaza ni kwamba mzunguko wa kwanza kulikuwa na waamuzi wengi wapya wakiwamo wa kike ambao tunachelea kusema kwa kiasi fulani walichezesha vizuri, na hata makosa yaliyoonekana mashabiki wengi waliamini kuwa ni ya kibinadamu.

Ukweli ni kwamba mashabiki wengi wa soka nchini wanajua kama makosa anayofanya mwamuzi ni ya makusudi au ya bahati mbaya kwa sababu wanaangalia soka kila uchao kwenye Ligi Kuu sehemu mbalimbali duniani kupitia runinga.

Huwezi kuwadanganya, ndiyo maana mashabiki wa Simba walicharuka baada ya mechi dhidi ya Azam pale mwamuzi Ramadhani Kayoko aliposhindwa kumudu mchezo huo dhahiri.

Ni hawa hawa mashabiki ambao mechi nyingi nyuma hawakuwagusa waamuzi, badala yake walililalamikia benchi lao la ufundi, baadaye wachezaji wao tena katika mechi ambazo timu yao wakati mwingine inapata ushindi.

Kitendo cha kumnyooshe kidole cha shahada mwamuzi, Kayoko na maneno mengi ya vitisho, kisichukuliwe kawaida na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), badala yake waone wana kazi ya kufanya ili kurekebisha hali ya mambo kabla haijawa mbaya siku moja, ingawa kwetu sisi tunasimamia mstari wa mbele kukemea hali mbaya isijeikajitokeza.

Ikumbukwe mchezo wa mpira mara nyingi hubebwa na hisia kubwa zikiandamana na damu kuchemka, hivyo waamuzi nao wanapaswa kulitambua hilo kwa kuongozwa sheria 17 za soka na haki na si vinginevyo.

Kama mzunguko wa kwanza walichezesha waamuzi wengi walisiokuwa na uwezo, lakini hakukuwa na malalamiko, kwa nini sasa hivi baadhi ya waamuzi wazoefu wamerejea kelele zimeanza?

Ikumbukwe Kayoko ni mmoja wa waamuzi ambao walifungiwa na baada ya hapo hakusikika kelele za aina hii kwa waamuzi chipukizi ambao kwa waliochezesha ligi, kiasi cha hata TPLB yenyewe kusifia.

Maamuzi ya uchezeshaji mbovu wa waamuzi wetu kwa sasa katika mechi mbalimbali za hivi karibuni yamekuwa wakipostiwa na waandishi nguli barani Afrika kwenye mitandao ya kijamii kiasi cha kuwa ni ushahidi wa kwa nini waamuzi wetu hawaendi kuchezesha AFCON.

Hii si dalili nzuri kwa ligi yetu ambayo imepiga hatua nyingi mbele ikiwa nafasi ya tano kwa ubora, lakini baadhi ya waamuzi wanataka kuirudisha nyuma kwa nia zao ovu.

Tunaiomba Bodi ya Ligi kutoa adhabu kali kwa waamuzi wote wanaotaka kuharibu ladha ya ligi hasa wakati huu wa kuelekea kumpata bingwa. Imefika wakati sasa kamati iwashushe daraja waamuzi wanaovurunda kwenda kuchezesha Ligi ya Championship kwa msimu mzima.

Pia iwaondoe kabisa kuchezesha soka waamuzi ambao wana makosa ya kujirudia. Haiingii akilini mwamuzi mwenye beji ya FIFA anafungiwa, akifunguliwa mechi chache tu, anafanya makosa yale yale.

Tumekuwa tukipigia kelele vitu vingi ambavyo vimekuwa vikilikwamisha soka la Tanzania, miongoni mwa ambavyo wengi hawavitolei macho ni waamuzi.

Baadhi waonekana kutengeneza matokeo ambayo si sahihi kwa timu zingine. Timu iliyostahili kufungwa inashinda au kutoa sare hapa hatuusaidii mpira wa Tanzania.

Tunapata wachezaji wa timu ya taifa wasiostahili kwani wanaonekana kucheza vizuri, lakini kumbe kuna wachezaji wengine wazuri hawaitwi kwa sababu tu timu zao zinanyongwa na waamuzi na kuonekana hawana uwezo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Simba, Yanga na hekaya 'mfu' za uwanja wa kisasa

**TANGU** nilipoanza kufuatilia masuala la soka zaidi ya miaka 30 iliyopita, sijaacha kuisikia kauli ya 'tutajenga uwanja wa kisasa.'

Kauli hii nilianza kuisikia miaka ya 1980 wakati wa kuomba kura ya kuwa viongozi kwenye klabu kubwa za Simba na Yanga.

Wakati huo nafasi zilikuwa ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Katibu Mkuu Msaidizi, Mweka Hazina, Mweka Hazina Msaidizi na Katibu Mwenezi.

Viongozi waliokuwa wanaomba wanachama kura zao moja kati ya ahadi zao ilikuwa ni kuzijengea timu uwanja. Hata hivyo hakuna uwanja uliokuwa unajengwa, na ahadi hizo ndizo zilikuwa zinawaondoa madarakani iwe kwa kura au mapinduzi (wakati huo), lakini cha ajabu nao waliokuwa wakiingia walifanya vile vile kama waliotangulia.

Nao waliahidi kujenga viwanja na hawakufanikiwa, nadhani kwa bahati mbaya au makusudi. Nikisema makusudi ni kwamba wapo waliokuwa wakisema tu kuwa watajengwa uwanja, lakini hawakuwa na dhamira ya kweli.

Waliitumia ahadi hiyo kama chambo tu cha kuingilia madarakani kwa sababu wanachama walikuwa na hamu ya kuona klabu zao siku moja zinakuwa na viwanja vyao.

Inawezekana wapo walioingia wakiwa na dhamira ya kweli, lakini wanachokutana nacho wanapokuwa madarakani wakagundua kuwa ni mgumu na haiwezekani kirahisi hivyo.

Mwenyekiti wa klabu ambaye anaingia madarakani kwa miaka mitano tu, halafu hana uhakika wa kushinda uchaguzi ujao, anajengaje uwanja wa soka ambao ujenzi wake unaweza kuchukua hata miaka miwili au mitatu?

Je, akijenga yeye atafaidika nini wakati anaweza kuondolewa madarakani kwenye uchaguzi unaofuata? Na siyo hivyo tu, wakati huo kulikuwa na tabia ya kuondoa viongozi madarakani kwa nguvu. Wanaitana wanachama klabu ni na kutangaza mapinduzi, mwenyekiti yeye au na watu wake wasionekana klabuni na hawatakiwi kuigusa timu.

Hii ilisababisha kuingia watu wanaitwa wafadhili. Lakini nao walitoa pesa zao kwa ajili ya kambi, chakula na usafiri kwa wachezaji, lakini siyo kujenga uwanja. Kujenga uwanja ni kitu kingine kabisa.

Kwa sasa wameingia wawekezaji. Nao pia wamekuwa na ahadi ya kujenga viwanja kila uchao. Nadhani hata wao wanasema hivyo kwa sababu ile ile ya wale viongozi wa mwanzo. Wawekezaji hawa bado hawajazishika klabu kisawasawa ili kuweza kufanya hivyo.

Kwangu mimi hata waseme vipi sioni dhamira ya dhati ya wao kujenga uwanja. Ndiyo maana utaona mashabiki wa Simba walichanga pesa, lakini zikaishia kuzungushiwa uzio kwenye Uwanja wa mazoezi Bunju.

Yanga nako, pamoja na kuwa wana eneo Kigamboni, lakini bado wanang'ang'ania kujenga pale Jangwani ambapo mvua ikinyesha unaona jinsi kunavyokuwa na matatizo ya miundombinu.

Imefika wakati serikali na hata wanachama wenyewe kukubali wawekezaji hawa kuwa na asilimia kubwa ya hisa.

Nina uhakika wakiwa na hisa nyingi na kuwa na uhakika, wanaweza kujenga uwanja na kuzipatia faida baadaye, lakini siyo kama hivi sasa ambapo hata uwekezaji wenyewe kukamilika umekuwa mtihani.

Wanahofia wanaweza kujenga, halafu ikala kwao, likaja jambo lolote ambalo linaweza kuwafanya waondoke kwa sababu hawana nguvu inayowalinda.

Kwa sababu hili la uwanja kwangu nimeanza kulisikia zamani sana, wala sishawishiki kama Simba na Yanga zitajenga leo wala kesho. Mpaka wawekezaji wahakikishiwe uwekezaji wenye tija na wenye faida si huu kama wa kusaidia tu.

Binafsi, naona litafanikiwa tu pale wanachama wenyewe wakiridhia kuwapa wawekezaji asilimia kubwa zaidi kuliko wao na serikali kuamua kwa dhati wawekeze kama wanavyofanya kwenye makampuni. Vinginevyo itabaki ni hadithi za kusadikika au zile za Alfu Lela Ulela, mazungumzo ya siku elfu moja na moja.

HABARI KITAIFA

# Madiwani wamkataa mkurugenzi

**Na Mwandishi Wetu,** NANYAMBA

MADIWANI wa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, mkoani Mtwara wameazimia kumkataa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba mkoani Mtwara, Thomas Mwailafu kwa madai kuwa hana ushirikiano na anahatarisha kura zao kwenye Uchaguzi Mkuu ujao.

Uamuzi wa madiwani hao ulifikiwa mwishoni mwa wiki baada ya baraza lao kujigeuza kuwa kamati kumjadili mkurugenzi huyo.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo ambaye hakuwa kikaoni, alipotafutwa alidai hakuwa ofisini na atakaporejea atatoa maelezo licha ya kutosikia malalamiko juu yake.

Akitoa maazimio ya baraza la madiwani, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Jamal Kapende, alisema walijadili mambo matatu ikiwamo utendaji kazi wa mkurugenzi ambapo madiwani walitoka na kauli ya kumkataa kwa madai kuwa hana ushirikiano na kupuuza ushauri wao.

"Utendaji wake ni kikwazo kwa madiwani, wanachokiona ni kwenda kufeli 2025 kwa kuwa wananchi watakuwa hawayaoni matokeo, niwaombe watendaji wa halmashauri kila mtu acheze kwa namba yake atoe pasi, lawama ziwe kwa mfungaji," alisema.

Kabla ya kufikia uamuzi huo, Diwani wa Nanyamba, Hassan Mauji, alidai kuwa kila wanapotaka kujadili utendaji wa mkurugenzi huyo na uhusiano na watumishi wa halmashauri hiyo, alizuia, hivyo akamwomba Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI kumwondoa mkurugenzi huyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Wakili Prosper Kisinini, alisema suala la baraza kujigeuza kuwa kamati ni kinyume cha taratibu na halina mamlaka ya kumjadili mkurugenzi huyo ambaye yuko chini ya mamlaka ya Katibu Mkuu TAMISEMI.

## TAKUKURU yanyatia nyendo za wala rushwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi, amewataka watumishi mkoani mwake kutotumia vibaya nafasi walizonazo, kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa wananchi wanaofika katika maeneo yao kupata huduma zikiwamo za matibabu.

Agnery Mganga alitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki alipozungumza na Nipashe ofisini kwake mjini Lindi.

Alikumbusha kuwa hivi karibuni taasisi huyo ilimkamata na kumfikisha mahakamani mtumishi wa Idara ya Afya anayehudumu Hospitali ya Mkoa wa Lindi (Sokoine), aliponaswa kwa kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 70,000 kutoka kwa mgonjwa hospitalini huko. Tayari hukumu dhidi ya mtumishi huyo imeshatolewa na mahakama.

Alisema TAKUKURU haitamfumbia macho mtumishi yeyote wa umma atakayebainika kushiriki kuomba na kupokea hongo kwa kuwa ni kinyume cha sheria.

Mganga aliwataka wananchi kutokubali kulipa fedha kupitia mtu binafsi, badala yake wafuate utaratibu uliowekwa na serikali wa kulipia kwa mfumo ulioandaliwa.

Februari 6, mwaka huu, katika jengo la Hospitali ya Sokoine mjini Lindi, daktari alikamatwa na maofisa wa TAKUKURU akipokea rushwa ya Sh. 70,000 kutoka kwa ndugu aliyemsindikiza mgonjwa hospitalini huko.

**Alisema TAKUKURU haitamfumbia macho mtumishi yeyote wa umma atakayebainika kushiriki kuomba na kupokea hongo kwa kuwa ni kinyume cha sheria.**




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako (katikati), akizungumza wakati akifunga kikao kazi cha mafunzo ya uelimishaji kwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania - Divisheni ya Kazi, Kanda ya Kusini, juzi. Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma (kushoto) na kulia ni Joseph Karayemaha, Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Kanda ya Songea. **PICHA: MIGAPICHA WETU**

# PAC yapongeza eGA kusimika mifumo ya TEHAMA serikalini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imepongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kwa kuokoa fedha nyingi za serikali zilizokuwa zinatumika kununua mifumo ya TEHAMA nje ya nchi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki baada ya kamati hiyo kutembelea Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC) cha mamlaka hiyo jijini hapa.

"Kamati yetu imefurahi, tumefundishwa kuangalia mabaya na ndio tumefundishwa hivyo, na kuyasemea madhaifu lakini katika hili tuwaongeze mmewezesha serikali kuokoa fedha nyingi kwa kusanifu na kutengeza mifumo ya TEHAMA inayotumika katika taasisi mbalimbali za umma ambayo hapo awali mifumo hiyo ilinunuliwa kutoka nje ya Tanzania kwa gharama kubwa," alisema.

Hasunga alisema taasisi mbalimbali za umma walizozitembelea siku za nyuma zilikuwa na tatizo la mifumo ya Tehama, lakini kwa sasa zimeimarika kutokana na kazi iliyofanywa na eGA.

"Moja ya jambo lililokuwa linatusumbua sana kamati hii ni taasisi nyingi kununua mifumo ya TEHAMA kutoka nje, lakini msimbo (source code) unabaki kule kwa waliotengeneza mifumo na wakati mwingine mifumo hiyo baada ya muda haitumiki tena na hivyo sisi tumekuwa tunasema hakuna thamani ya fedha katika ununuaji mifumo hiyo ambayo tumetumia gharama kubwa sana kuinunua.

"Kuna taasisi zilinunua mifumo kwa zaidi ya Sh. bilioni 30, lakini mfumo haujamaliza mwaka wanautupa na tulipowauliza walisema waliona mfumo huo haufai, hivyo wameamua kutafuta mfumo mwingine. Sisi tunasema hakukuwa na thamani ya fedha," alisema.

Alitaka mamlaka hiyo kuhakikisha taasisi nyingi zaidi zinaunganishwa katika Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (GovESB), ili kurahisisha upatikanaji huduma za serikali mtandao kwa wananchi.

"Tumefurahi sana kuona namna mifumo mbalimbali inavyowasiliana, tujitahidi tufike angalau asilimia 80 tu tutakuwa tumefika pazuri kwa sababu tutapunguza gharama na malalamiko katika utoaji huduma za serikali mtandao," alisema.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, alisema kituo hicho kwa sasa kinakabiliwa na ufinyu wa eneo, hivyo eGA inahitaji kutengewa bajeti ili kujenga miundombinu (majengo) yake katika eneo la Kikombo.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa eGA, Benedict Ndomba, alishukuru kamati hiyo kutembelea kituo hicho na kuahidi kutekeleza maelekezo, maoni na ushauri uliotolewa na wajumbe wa kamati hiyo ili kuimarisha ubunifu na utafiti wa serikali mtandao.

# Akaunti ya NMB isiyo na makato ya mwezi yapokewa kwa shangwe

**Na Mwandishi Wetu**

MAELFU ya wananchi wa Wilaya ya Temeke, hususani wakazi wa Mbagala na vitongoji vyake, mwishoni mwa wiki walifurika katika tamasha la kuhamasisha ufunguaji akaunti nafuu isiyo na makato ya mwezi inayotolewa na Benki ya NMB lililopewa jina la NMB Pesa Day.

Tamasha hilo lilifanyika kwenye Viwanja vya Mbagala Zakhiem, likienda sambamba na uzinduzi wa kampeni ya Weka na Ushinde itakayodumu kwa miezi mitatu, mgeni rasmi akiwa Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda.

Katika tamasha hilo lililotanguliwa na mbio za taratibu 'jogging' na burudani za muziki kutoka kwa wasanii kama Miso Misondo na Wazee wa Makoti, Mr Blue, Dulla Makabila na wengineo, Mapunda alipongeza NMB kwa ubunifu katika kusambaza huduma jumuishi za kifedha kwa wananchi.

Mapunda alisema NMB Pesa inakwenda kuwa chachu ya maisha bora kwa wana Temeke na watanzania kwa ujumla, ambako licha ya 'jogging,' wahudhuriaji walipewa elimu na huduma za kifedha, mashindano ya vipaji vya muziki, ambako zawadi mbalimbali zilitolewa na kiongozi huyo kwa washindi.

"Tupo hapa kwa ajili ya NMB, ambayo inafanya kitu kikubwa sana leo kwa ustawi wa maisha yetu. Kwa kutuletea NMB Pesa, ambayo kwa Sh. 1,000 tu, unafungua akaunti hata ukiwa na simu ya kitochi, akaunti ambayo itakuwezesha kupata huduma zote za kifedha, ikiwamo mikopo, kutuma, kupokea, kutoa fedha na kulipia bili mbalimbali.

"Sasa, mimi niwaombe kitu kimoja wana Mbagala, sisi tupo wengi sana na 'buku buku' (1,000/-) zipo nyingi sana miongoni mwenu, changamkieni fursa kwa kufungua akaunti za NMB Pesa ili mjiwekee akiba, lakini mpate kunufaika na huduma za kifedha za benki hii.

"Hapa kuna droo nyingi zinaendelea kwa wote wanaofungua akaunti sasa, ambapo watajishindia fedha taslimu, majiko na mitungi ya gesi, baiskeli za tairi tatu 'guta,' na zawadi kubwa zaidi ya bodaboda ambayo nitaikabidhi mwishoni mwa tamasha hili. Kwahiyo, changamkieni fursa," alihimiza.

Awali Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna aliwahakikishia wananchi wa Mbagala na Watanzania kwa ujumla kwamba NMB imewaletea fursa inayokwenda kubadili maisha yao, kupitia NMB Pesa Akaunti, ambayo ni ya kidigitali unayofunguliwa kwa Sh. 1,000 tu, ikiwafikia ikiwa na fursa nyingi.

"Fursa ya kwanza inayokuja na akaunti hii ni kuwa unaingia moja kwa moja kwenye huduma jumuishi za kifedha kupitia NMB, watoa huduma wametapakaa kote kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa sehemu ya huduma hii inayokuja chini ya kaulimbiu ya 'Haachwi Mtu.'

"Kupitia NMB Pesa, utakuwa umeingia moja kwa moja katika huduma ya NMB Mkononi, inayokupa wigo mpana wa kujihudumia na kuhudumiwa kibenki bila kuja kwenye matawi ama katika ofisi za benki yetu ambako utafanya miamala na malipo na manunuzi kidigitali.

"Pia rekodi zako kipesa kupitia NMB Pesa Akaunti zitakuongezea fursa kwani kubwa kuliko yote utaweza kukopa hadi Sh. 500,000 kupitia Mshiko Fasta, huduma ya mikopo isiyohitaji dhamana yoyote wala kujaza fomu. Hapo vipi, haujabadilisha maisha yako?

"Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, hii kampeni tunayoianza leo, ni kampeni ya Weka Akiba na Ushinde. Kwa hiyo, pamoja kufungua akaunti ya NMB Pesa, lakini tunazindua kampeni ya Weka Akiba na Ushinde, yaani unaweka Sh. 50,000 na unajishindia zawadi mbalimbali," alisisitiza.

Zaipuna alibainisha kwamba kila wiki kutakuwa na droo zitakazozalisha washindi 10 wa watakaojishindia Sh. 500,000 kila mmoja, washindi watano wa kila mwezi watazoa Sh. milioni moja na katika droo ya fainali, mshindi atajinyakulia Sh. milioni 10, washindi wanane wa Sh. milioni tatu, mashine ya kufulia, Tv, friji, bodaboda tano na pikipiki nane za mizigo.

"Kwa mantiki hiyo, tunawakaribisha Watanzania wote wajiwekee akiba, lakini wabadilishe maisha na kuboresha biashara zao kupitia akiba na zawadi watakazoshinda," alisema Zaipuna alipozungumza na maelfu ya waliohudhuria tamasha hilo, lililofungwa kwa Agnes Maujundu kujinyakulia bodaboda.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kushoto), akimkabidhi zawadi ya bodaboda Agnes Maujundu (katikati), baada ya kushinda shindano la kufungua akaunti ya NMB wakati wa tamasha la kuhamasisha wananchi kufungua akaunti ya NMB Pesa kwa Sh. 1,000 Mbagala Zhakem jijini Dar es Salaam. Kulia ni Ofisa Mkuu Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi. **PCHA: MPIGAPICHA WETU**

## Sababu kuu vyura wa Kihansi kutorejeshwa mazingira yao ya asili

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MATOKEO ya awali ya tathmini ya sababu zinazozuia urejeshwaji vyura wa Kihansi katika mazingira yake ya asili, yanaonesha kuwapo shida katika ubora wa maji ya Bonde la Kihansi.

Bunge limeelezwa kuwa maji hayo yana kiwango kikubwa cha amonia ambacho kinaweza kuwa chanzo cha ustawi hafifu wa vyura katika eneo hilo.

Kwa sasa utafiti wa vinasaba unaendelea ili kubaini kama kuna mabadiliko ya vinasaba yanayosababisha kufifia kwa ustawi wa vyura hao.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, iliyowasilishwa bungeni wiki iliyopita na Mwenyekiti wake, Timotheo Mnzava, tathmini hiyo inafanyika chini ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI).

Wakati anawasilisha taarifa ya shughuli za kamati hiyo kwa mwaka 2023, Mnzava ambaye pia ni Mbunge wa Korogwe Vijijini (CCM), alisema katika kipindi cha mwaka 2022/23, taasisi hiyo ilifanya utafiti unaogusa jamii, ikiwa ni pamoja na tathmini hiyo.

"Utafiti huo unahusu sababu zinazozuia urejeshwaji chura wa Kihansi katika mazingira yake ya asili.

"Katika kufanya tathmini ya sababu hizo matokeo ya awali yanaonesha maji katika Bonde la Kihansi yana kiwango kikubwa cha amonia ambacho kinaweza kuwa chanzo cha ustawi hafifu wa vyura katika eneo hilo," alisema.

Alisema TAWIRI ndio tegemeo katika sekta ya uhifadhi na utalii nchini, lakini inakabiliwa na changamoto ya ukosefu rasilimali fedha inayotokana na ufinyu wa bajeti, hali inayoathiri utekelezaji majukumu yake kwa ufanisi.

Taasisi hiyo pia haina jengo la makao makuu tangu ilipoanzishwa mwaka 1980 na inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu, uhaba wa vifaa vya kisasa katika utafiti na ukosefu wa fedha za sensa za wanyamapori.

# OSHA yasifu matumizi ya TEHAMA kurahisisha usimamizi usalama, afya

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umeeleza kuwa matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) umeiwezesha kupata taarifa muhimu kuhusiana na mtawanyiko wa shughuli za kiuchumi nchini.

Uongozi wa wakala huo umesema kuwa kupitia TEHAMA, umeandaa mipango madhubuti ya kulinda nguvukazi inayotumika katika shughuli husika dhidi ya vihatarishi vya magonjwa na ajali mahali pa kazi.

Jijini Arusha mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa taasisi hiyo, Raymond Machary, alibainisha hayo alipowasilisha mada kuhusu umuhimu wa TEHAMA katika usimamizi wa masuala ya usalama na afya katika maeneo ya kazi. Machary alisema OSHA imepiga hatua kubwa katika matumizi ya TEHAMA, inao mfumo wake wa ndani wa usimamizi wa taarifa za maeneo ya kazi (Workplace Information Management System) ambao umeunganishwa na mifumo mingine ya serikali ukiwamo mfumo wa Malipo ya Serikali (GePG).

"Kupitia matumizi ya mfumo wetu wa WIMS na mifumo mingine ya serikali, taasisi yetu imeweza kukusanya na kuhifadhi taarifa muhimu kuhusiana na shughuli za kiuchumi zinazofanyika nchini, jambo ambalo linarahisisha usimamizi wa masuala ya usalama na afya katika maeneo ya kazi husika.

"Vilevile, kupitia mfumo huo wadau wetu wanaweza kupata huduma zetu ikiwamo usajili wa maeneo yao ya kazi bila kulazimika kufika katika ofisi za OSHA.

"Mathalani sisi OSHA tunao uwezo wa kutoa taarifa za miradi ya ujenzi yote inayoendelea nchini wakati wowote ambapo kwa sasa mkoa wenye miradi mingi ni Dar es Salaam ukifuatiwa na Dodoma na Arusha, jambo ambalo lilikuwa haliwezekani kabla ya kuwekeza katika mifumo ya TEHAMA," alisema.

Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja (Director of Corporate Services) wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Salum Rugambwa, alipongeza OSHA kwa kuwa mstari wa mbele katika matumizi ya TEHAMA.

"OSHA wanao mfumo wao wa ndani ambao waliutengeneza kwa kuzingatia taratibu zote za serikali zinazosimamiwa na eGA na sisi kama wadhibiti wa serikali mtandao tunaendelea kushirikiana nao pamoja na taasisi nyingine za umma ili kuhakikisha kwamba mifumo iliyopo inafanya kazi kwa ufanisi ikiwamo wataalamu wetu kutoa msaada pale mifumo inapopata changamoto," alisema Rugambwa.



## Mkakati kuboresha reli kuunganisha bandari

**Na Hamida Kamchalla,**
TANGA

WIZARA ya Uchukuzi bara na Wizara ya Uchukuzi, Mawasiliano na Usafirishaji ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekutana jijini Tanga katika mkutano wa pili wa ushirikiano na kutembelea Bandari ya Tanga kuona ufanisi wake.

Akiwa katika ziara ya kukagua Bandari ya Tanga, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, alisema serikali imeanza kutekeleza mradi maalumu wa kuboresha reli ya Dar es Salaam kwenda mikoa ya Kaskazini ili kurahisisha usafiri kwa upande wa bandari nchini.

Aidha, aliutaka uongozi wa Bandari ya Tanga kutenga bajeti ya maboresho ya reli inayoingia bandarini humo kwakuwa lengo la serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuendeleza bandari zote nchini kwa manufaa ya uchumi wan chi.

"Na hapa Tanga kuna mradi maalumu wa kufufua reli hii ya Kaskazini kipande cha takribani kilomita 435 kutoka Dar es Salaam kwenda mikoa ya kaskazini ambayo inapita hapa na tayari tumeshapewa fedha na serikali na maboresho yameanza kufanyika.

"Tumeshaanza kwa kung'oa vyuma ili iweze kuhimili mizigo mizito lakini mwendo wa treni uongezeke, hii itafanya kuwa rahisi sana kuchukua mizigo kupeleka Dar es Salaam na itakuwa msaada mkubwa kwa kuisaidia Bandari ya Dar es Salaam," alisema.

Mbali na hilo pia aliutaka uongozi huo kuitangaza fursa za Bandari ya Tanga badala ya kuangalia na kutangaza vitu vingine vilivyopo na kwa kuboresha reli usafiri wa kutoka Tanga kwenda Dar es Salaam utakuwa ni rahisi.

Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi, Mawasiliano na Usafirishaji kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Khalifa Khamis Rajab, alisema lengo la mkutano huo ni kuendeleza ushirikiano baina yao kwa kuwa kazi inayotekelezwa ni moja katika kuwahudumia wananchi.

Kaimu Meneja wa Bandari ya Tanga, Peter Milanzi, alisema matarajio ya kufunguka kwa Mkoa wa Tanga kupitia bandari hiyo ni makubwa na mradi wa uboreshaji umekamilika mwishoni mwa mwaka jana.

"Tunapokutana katika vikao vyetu huwa kuna baadhi ya vitu ambavyo vinaleta matatizo kati ya nchi hizo mbili, kwahiyo tunajadili na kuviweka sawa," alisema.

Pia Milanzi alifafanua kwamba tayari wameshaanza kupokea oda za kampuni kubwa kutoka nje ya nchi kutokana na uvoreshwaji mkubwa uliofanywa katika bandari hiyo.

"Mzigo mkubwa unaopita kwa sasa ni Amonium Nitrate, zao la mkonge, mafuta pamoja na malighafi za viwandani lakini pia mitambo ya viwanda hivyo, na timu yetu ya masoko inafanya kazi kubwa ya kuhakikisha wateja wanatumia bandari yetu ya Tanga," alisema.

# Haki Madini yawanoa wanawake wajasiriamali

**Na Cynthia Mwilolezi,**
SIMANJIRO

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Haki Madini, limewanoa wadau wanawake 21 wanaofanyakazi katika sekta ya madini ya tanzanite, ili wazalishe kwa ubora na kutambua stahiki zao.

Wadau hao ni mawakala, waongeza thamani, wachekeshaji, wauza magonga (mabaki ya madini) na wajasiriamali.

Ofisa Miradi wa Shirika la Haki Madini, Emmanuel Mbise, alisema mafunzo hayo ya siku 10 yanayofanyika Mji Mdogo Mererani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, ambayo yatawajengea uwezo wanawake hao waongeze pato lao.

Alisema ni muda mrefu wanaume wamenufaika zaidi na sekta ya madini, hivyo wamewajengea uwezo wanawake hao ili na wao wanufaike kupitia kuongeza thamani ya madini na vito.

"Serikali imetenga eneo la Mji Mdogo wa Mirerani, liwe la kuongea thamani madini ya tanzanite na vito na sisi tukaona tutumie fursa hiyo kuwajengea uwezo wanawake wasiachwe nyuma washiriki kwa ujumla," alisema.

Ofisa Madini Mkazi (RMO) Mirerani, Nchagwa Marwa, akifungua mafunzo hayo aliwataka wanawake hao kuyatumia mafunzo kwa manufaa kwa kuwa yatawaongezewa uwezo.

Aidha, Marwa aliwapongeza Haki Madini kwa kuandaa mafunzo hayo yatakayowanufaisha wanawake wa eneo hilo.

"Ni fursa kubwa na nzuri mmepata wanawake wadau wa madini kupitia Shirika la Haki Madini, hivyo tuyatumie ipasavyo kwa kuleta mabadiko mtakapohitimu," alisema Chacha.

Ofisa Madini Jinsia wa Shirika Haki Madini,Joyce Ndakaru, alisema mafunzo hayo yamelenga la kuongeza ushiriki wa wanawake na unufaikaji kupitia madini ya tanzaniti na vito.

Alisema dhana ya kuwa sekta ya madini inahitaji nguvu pekee siyo sahihi, kwa kuwa ina lenga wanawake kuhakikisha wanashiriki na kunufaika na madini ya tanzaniti kupitia kuyaongeza thamani.

Alisema maendeleo kwenye sekta hiyo, yatapatikana endapo wanawake wakiingia kwenye kuongeza thamani wakitumia nguvu ya akili na sio nguvu ya mwili pekee.

"Wanawake wakiwa waelewa wa sekta husika wataweza kuongeza thamani ya madini kwa manufaa yao wenyewe na jamii inayowazunguka kwa ujumla," alisema.

Mmoja kati ya washiriki wa mafunzo hayo, Rachel Njau, aliwashukuru Haki Madini kwa kufanikisha mafunzo hayo kwa wanawake wadau wa madini ya tanzaniti.

Njau ambaye ni Katibu wa Chama cha Wachimbaji Madini mkoani Manyara (MAREMA),Tawi la Mirerani, alisema wanawake hao watayatumia mafunzo hayo kwa kunufaika zaidi tofauti na awali kabla ya kupata mafunzo hayo.



Wanachama wa vikundi vya Mfuko wa Kutunza Bahari (MKUBA) Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga, wakishika mfano wa hundi ya Sh. milioni 10.5 zilizotolewa na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) na viongozi wa Shirika la Mwambao Coastal Community Network linalojihusisha na utoaji elimu na uhifadhi wa mazingira baharini mwishoni mwa wiki. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Viongozi wanaopora ardhi kuchukuliwa hatua

**Na Hamida Kamchalla,**
HANDENI

SERIKALI wilayani Handeni, mkoani Tanga, imeahidi kuwashughulikia viongozi wa chama na watumishi wa serikali ambao wanadaiwa kupora ardhi iliyokuwa ikimilikiwa kihalali na wananchi ili irudishwe kwa wahusika.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Albert Msando, aliyasema hayo mbele ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Abdalla Rajabu, katika mkutano wa hadhara wa chama hicho wilayani humo.

Alisema kuna baadhi ya migogoro ya ardhi imesababishwa na baadhi ya viongozi kwa kuwafidia wananchi maeneo yao kwa fedha kidogo na baadaye kuviuza kwa fedha zaidi kwa wananchi wenye fedha lakini pia hata viongozi wenyewe.

"Mimi nikiwa kama serikali nasema kwamba wale viongozi wote, watumishi wa serikali lakini hata wabunge na madiwani mliochukua maeneo ya wananchi na kuyauza na kujimilikisha, ni lazima mtayatema,"alisema.

Kuhusu mgogoro wa tangu 1991 hadi sasa wa Shule ya Kata ya Chanika ambao hadi sasa haujakamilika mbali na viongozi mbalimbali wa serikali kutoa maelekezo alisema;

"Lakini mbali na maelekezo yote yaliyotolewa, aidha hayakutekelezwa au yalitekelezwa nusunusu au tofauti, mheshimiwa mwenyekiti eneo linalozungumziwa lilitengwa kwa ajili ya matumizi ya umma mwaka 1976.

"Eneo lilipangwa kwa ajili ya kujengwa Posta, lakini matokeo yake mwaka 1991 lilitolewa kwa mfanyabiashara na kujulikana kama Yakundi Interprises na ilipofika mwaka 1997 ilitolewa hati kwa kampuni ya Yakundi Investment na lilipangwa kwa ajili ya matumizi ya umma," alisema.

Alisema badala ya kutumika ipasavyo, lilipangwa kujengwa viwanda vidogo vidogo, na kwamba alipokuja Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mwaka 2020, aliagiza eneo lile lirudi shuleni, lakini badala yake ukaanza mpango wa kubadilisha matumizi.

"Alipoondoka Waziri Mkuu, eneo lile badala ya viwanda vidogo vidogo tena kulianzishwa matumizi maalumu na kilichotokea kukajengwa maduka ya biashara, kimsingi maelekezo yalitolewa na kiongozi mkuu ya kutaka eneo lirudishwe shuleni na mwekezaji apewe eneo jingine mbadala hayakutekelezwa" alisema.

Aidha, Msando alifafanua kero kubwa zinazoonekana kuwa sugu wilayani humo ni pamoja na barabara za ndani ya kata na mitaa, lakini pia umeme kukatika bila taarifa kutoka TANESCO.


"Kero nyingine ni maji, pamoja na kwamba serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya miradi mikubwa ya maji, Segera na Kabuku, mradi wa miji 28 na mradi wa visima virefu, lakini bado tuna kero kubwa ya maji na yanayopatikana ni ya chumvi," alisistiza.

Wakili Msando alibainisha kwamba, "Ili Wakurugenzi waweze kufanya kazi zao ipasavyo ni lazima washirikiane na mabaraza ya madiwani".

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Handeni, Amiri Changogo, alisema migogoro ya kata ya Chanika inafahamika kwa muda mrefu na kwamba chama kimeshaanza kuchukua hatua za utatuzi.

"Na tulimpa wiki mbili mkuu wa wilaya na watendaji wake watuletee majibu na wiki mbili hizi zinaisha Februari 13, hivyo tunaamini Wakili Msando ambaye mimi namuamini sana, atatuletea majibu kamili kuhusu migogoro yote iliyosemwa hapa," alisema Changogo.

Na kati ya migogoro hiyo upo pia ule wa kata ya Mgambo, ambayo pia imeunganisha Jeshi letu la Mgambo kule (JKT) na vijiji vya Kwankonje na Komsanga, nikuombe sana Mwenyekiti, hiyo yote ataitekeleza migogoro hiyo mpaka kufikia Februari 13, mwaka huu ni lazima tupate majibu ya migogoro hii," alisisitiza.





# Familia yafunga matanga bila kuona, kuzika mwili

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MTOTO Salumu Matheo (11), mkazi wa Mtaa wa Mbuyuni, Kata ya Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga aliyedaiwa kufariki dunia kwa kuzama katika Mto Mhumbu alikokwenda kuvua samaki na kuogelea, ameibua jambo jipya:

Familia yake imeamua kuhitimisha msiba bila kupata mwili baada ya juhudi za kuutafuta majini kwa zaidi ya siku nane kugonga mwamba.

Tukio la mtoto huyo kudaiwa kufa maji lilitokea Februari 4, mwaka huu saa 12 jioni, akidaiwa alikwenda na wenzake watatu kuvua samaki na kuogelea katika Mto Mhumbu. Alizama huku marafiki zake wakikimbia kwenda kutoa taarifa kwa ndugu zake.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Matheo Peter, alisema jana kuwa imewabidi kuhitimisha msiba huo bila kufanya mazishi ya mwanawe, kwa kuwa siku zinaendelea kupita, hawana budi kuendelea na shughuli zingine.

"Tangu siku ya tukio, Februari 4, mwaka huu, tulitangaza msiba, familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wamekuwa wakija kuomboleza na sisi wakati tukiendelea kuutafuta mwili wa mtoto wangu ndani ya maji, lakini hakuna mafanikio ndipo tukaona tusitisha msiba hadi pale mwili wake utapopatikana," alisema Matheo.

Alishukuru Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na wananchi kwa jitihada zao walizozifanya kutafuta mwili wa mtoto wake ndani ya maji licha ya kutofanikiwa kuupata.

Bibi wa mtoto huyo, Mariamu Juma, alisema yote yaliyotokea wanamwachia Mungu na kutoa wito kwa wananchi ambao wako jirani na mto huo, wakiona mwili wa mjukuu wake, watoe taarifa kwa viongozi wa maeneo yao ili ziwafikie na kufanya taratibu za mazishi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Tambukaleli, Kata ya Ndembezi, Japhet Kisusi alisema tayari alikwishawasiliana na viongozi wenzake ambao wako pembezoni na mto huo, wakisikia kuna mwili wowote umeonekana wampatie taarifa.

Sheikh Hamis Nkingo wa Msikiti wa AQSWA ambaye alihitimisha msiba huo kwa dua, alisema kwa taratibu za kidini kikipatikana hata kiungo chake kimoja, kitafanyiwa taratibu zote za mazishi kwa kuwakilisha mwili mzima na kuustiri kwenye makazi yake ya milele.



Imamu wa Msikiti wa AQSWA uliopo Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, Hamis Nkingo, akiendesha dua ya kuombea wazazi na familia ya mtoto Salumu Matheo (11), ambaye alizama ndani ya mto Mhumbu baada ya kusitisha msiba wa mtoto huyo bila ya kufanya mazishi juzi kutokana na mwili wake kukosekana ndani ya maji tangu Februari 4, mwaka huu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mifuko 600,000 ya mbolea ruzuku yapelekwa Ushetu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Ushetu wilayani Kahama, mkoani Shinyanga imepokea mbolea ya ruzuku tani 30,000 sawa na mifuko 600,000 yenye thamani ya Sh. bilioni 49.

Kupokewa kwa mbolea hiyo kunatarajiwa kusaidia kuinua uzalishaji mazao ya chakula na biashara katika halmashauri hiyo.

Akithibitisha kutolewa mbolea hiyo kwa ajili ya msimu wa kilimo wa 2023/24, Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Charahani alisema mbolea hiyo inajumuisha tani 25,000 sawa na mifuko 500,000 kwa ajili ya wakulima wa tumbaku.

Alibainisha hayo alipozungumza na wananchi wa Kijiji na Kata ya Igwamanoni baada ya ugawaji dawa na harambee ya ujenzi wa mabweni katika Shule ya Sekondari Igwamanoni.

Mbunge huyo alisema wanatarajia uzalishaji wa mazao ya chakula, mikunde na biashara utaongezeka kutokana na serikali kuwajali wakulima kwa kuwapatia pembejeo kwa wakati na kuwataka wakulima kuzingatia kilimo chenye tija.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alisema mkoa umepokea Sh. bilioni 27 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kilimo ikiwamo ujenzi wa mabwawa makubwa mawili ya kilimo cha umwagiliaji na kuwataka wakulima kuhifadhi chakula baada ya mavuno na si kuuza chote ili kukabiliana na upungufu wa chakula ndani ya familia zao.

Alisema mabwawa hayo yanajengwa katika Kata ya Nyida wilayani Shinyanga na Kijiji cha Malenge wilayani Kahama.

Alisema watanunua pia pikipiki 224 kwa ajili ya maofisa ugani ambao watakuwa wanatembelea wakulima na kuwapatia elimu ya namna ya kulima kisasa na si vinginevyo.

Mkulima wa Sabasabini, Jumanne Hamisi, alisema msimu huu mbolea iliwafikia kwa kiwango kikubwa ikiwamo ya kukuzia na kupandia.

## Wakusanyaji mapato halmashauri kupimwa kila baada ya miezi 3

**Na Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

HALMASHAURI ya Buchosa, wilayani Sengerema, mkoani Mwanza imetoa muda wa kila baada ya miezi mitatu kuwakagua na kuwafanyia tathmini wakusanyaji mapato endapo hawatafikisha malengo ndani ya kipindi hicho, wataondolewa katika nafasi zao.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Buchosa, Idama Kibanzi, alitangaza hatua hiyo juzi katika Mkutano wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kujadili mapendekezo ya mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Alisema kuwa kwa mwaka huu wa fedha wamekusanya mapato zaidi ya asilimia 72 kutokana na ushirikiano pamoja na kufanya kazi kwa umoja ili kufikia malengo ya kukusanya mapato zaidi ya kiwango walichojiwekea.

"Ili tufikie malengo, kwa kipindi hiki hatutokuwa na huruma kwa wakusanyaji ushuru wasiofikia malengo tunayojiwekea, hivyo tutahakikisha kila baada ya miezi mitatu tunafanya tathmini na kuondoa wale walioshindwa kazi," alisema Kibanza.

Alisema kuwa katika bajeti ya mwaka 2024/25, wameweka vipaumbele ambavyo watafanya pindi watakapokuwa wanakusanya mapato yao na kusema watakuwa na miradi ya kimkakati kama vile ujenzi wa stendi, soko la kisasa na shule katika Kata ya Nyakasungwa ambako ujenzi tayari umeanza.

Mkurungezi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Bensoni Mihayo, alisema katika ukusanyaji mapato wameunda kikosi kazi kwa ajili ya kufuatilia na kuhakikisha ukusanyaji mapato unaongezeka na si kupungua.

Alisema hatua hiyo tayari imeanza kutekelezwa ambapo tayari wakusanyaji mapato 10 wameondolewa kwa kukusanya kiasi kidogo cha mapato.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, aliagiza baraza hilo kupitia mkurugenzi pamoja na mwenyekiti wa baraza kuendeleza ushirikiano na kuhakikisha wanabuni miradi zaidi ili wafikie malengo.

Kikao hicho kilipitisha makadirio ya bajeti ya Sh. bilioni 4.29 kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Nipashe
Spotika




USAJILI WA DIRISHA DOGO ULIOANZA KULIPA LIGI KUU UK. 14

# KLABU ANAZOWEZA KWENDA VAN DIJK




Virgil van Dijk

**LIVERPOOL, England**

KUONDOKA kwa Jurgen Klopp na maoni yaliyofuata kutoka kwa mlinzi Virgil van Dijk yametia shaka juu ya mustakabali wa muda mrefu wa Mholanzi huyo ndani ya Liverpool.

Katika mchezo wa kwanza baada ya Klopp kutangaza kuwa ataondoka mwishoni mwa msimu huu, Van Dijk alizungumza na waandishi wa habari, aliulizwa ikiwa kuondoka kunaathiri nia yake ya kubakia Liverpool. Jibu lake lilikuwa wazi vya kutosha kuwafanya watu wafikirie kuwa kuhama majira ya joto ni jambo ambalo haliko mbali sana na uwezekano wake.

"Hilo ni swali kubwa. Naam, sijui," alijibu Mholanzi huyo. Mkataba wake, kama wachezaji wengine muhimu, utamalizika Juni 2025. Ukweli huu uliwekwa kwake na aliongeza mafuta zaidi kwenye moto kwa kusema: "Hiyo ni sahihi - hesabu nzuri! Sikiliza, sijui.

"Klabu itakuwa na kazi kubwa mikononi mwao. Hilo linajulikana. Kuchukua nafasi ya kocha na wafanyakazi wanaondoka, na kuna mambo mengi yatabadilika. Kwa hiyo klabu ina kazi kubwa mikononi mwake na nina nia sana ya kutaka kujua ni mwelekeo gani utaingia. Lakini hilo litakapotangazwa tutaona hali yetu. Siwezi kusema mengi kuhusu hilo."

Maneno hayo hayamaanishi kuwa anaondoka mara moja, na Klopp alikanusha maana inayodhaniwa, lakini inatosha kuzua uvumi juu ya wapi anaweza kwenda. Hizi hapa ni baadhi ya klabu ambazo zinaweza kuwa kwenye mfumo wake kama Van Dijk ataamua kuondoka wakati wa majira ya joto...

**Real Madrid**

Iliripotiwa na Marca baada ya mustakabali wa Van Dijk kutiliwa shaka kwamba Real Madrid wanaweza kuwa tayari kutoa nafasi ya kutua kwa Mholanzi huyo. Ni moja ya klabu chache duniani ambazo zinaweza kumvutia Van Dijk na kuweza kulipa aina ya mshahara ambao atautaka.

Real Madrid kwa sasa hawaongelei katika mabeki wa kati kutokana na majeraha. Eder Militao, David Alaba, Antonio Rudiger na Nacho Fernandez ndio mabeki wa kati wakuu katika klabu hiyo, hakuna hata mmoja wao anayetarajiwa kuondoka hivi karibuni.

Huenda Nacho akahamishwa ili kutoa nafasi kwa Van Dijk, lakini mchezaji huyo anaweza kuachwa kwenye benchi kila wiki kutokana na Real Madrid kucheza na mabeki wawili pekee wa kati. Hii inaweza kuwa fursa zaidi kama itatokea.

**Paris Saint-Germain**

Kumekuwa na matukio mengi katika miaka michache iliyopita ya Paris Saint-Germain kujaribu kumsajili Van Dijk, lakini beki huyo mara zote alitaka kubaki Liverpool. Bila kujali hilo, huwezi kamwe kuwatoa PSG wakati mchezaji huyo atakapokuwa anapatikana.

Wangekuwa na fedha za kumsajili na kumlipa, na ingawa wanaonekana kuwa na wachezaji wachanga katika madirisha ya hivi karibuni ya uhamisho, Van Dijk bila shaka angeboresha timu. Milan Skriniar hajakuwa mzuri kama walivyotarajia tangu alipowasili kutoka Inter Milan na sasa pia ana jeraha la muda mrefu, huku Presnel Kimpembe na Marquinhos pia wako chini ya kiwango cha Van Dijk.

**Barcelona**

Kwa hakika hili linaonekana kuwa gumu zaidi kwa mtazamo wa kifedha, lakini wanaweza kuweka dau la majumuisho machache. Barcelona hawataruhusu kabisa aina hii ya fursa kupita, na kuna sababu za kufikiria kwamba Van Dijk angefurahia harakati hii.

Akizungumza na Gary Neville kwenye kipindi cha The Overlap mwaka 2022 kuhusu uwanja wake wa ugenini anaoupenda zaidi kucheza, alifichua: "Ningesema Camp Nou, Barcelona. Ni wazi, kwangu mimi, nilitazama mechi nyingi za Barcelona nilipokuwa mdogo na kisha kuweza kucheza ndani yake lilikuwa jambo la kushangaza."

Wachezaji kama Ronald Araujo, Jules Kounde na Andreas Christensen wote ni mabeki wazuri, lakini si zaidi ya Van Dijk. Anaweza kuwa kiongozi katika timu. Uchumi unaweza kumshawishi kwenda PSG au Real Madrid, lakini kwa mapenzi yake yapo Barcelona.

**Chelsea**

Kama Barcelona, huwezi kabisa kuwatenga Chelsea katika hali kama hii. Hata kama inaonekana haitatokea kamwe, watalazimika kuchukua nafasi ya Thiago Silva wakati fulani. Wana mabeki wengi wa kati, lakini kama walivyoonesha kwa karibu kila nafasi kwa miaka kadhaa iliyopita, kuna nafasi ya mmoja zaidi.

Mabeki kama Trevoh Chalobah, Malang Sarr na Benoit Badiashile wote wanaweza kuwa hawapo msimu wa majira ya joto na kuwaacha Axel Disasi na Levi Colwill kama wachezaji ambao Mauricio Pochettino anawapenda. Wesley Fofana pia bado yuko klabuni na anajaribu kujiweka sawa.

Ikiwa Thiago Silva ataondoka kuna kundi la mabeki wachanga wenye vipaji ambao wanaweza kufaidika sana kutoka kwa mtu kama Van Dijk.

**Saudi Arabia**

Inaonekana mapema sana katika maisha ya Van Dijk kuondoka Ulaya, lakini labda ataondoka bila malipo mwaka wa 2025. Atakuwa na umri wa miaka 34 kufikia wakati huo.

Timu yoyote ya juu nchini Saudi Arabia itakuwa na fedha na nia ya kumsajili Van Dijk, lakini tahadhari ya Jordan Henderson inaweza kuwa ya kutosha kumweka mbali. Rufani bila shaka itakuwa siku kuu ya malipo mwishoni mwa kazi yake, lakini changamoto mpya barani Ulaya hakika inakubalika zaidi katika hatua hii.

## ISIKUPITE

MABAO mawili aliyofunga Erling Haaland kwenye mechi dhidi ya Everton juzi yanamfanya sasa kufikisha mabao 52 katika mechi zake 50 za kwanza za Ligi Kuu England. Hadi sasa msimu huu tayari amefunga mara 16 huku msimu uliopita akimaliza na mabao 36.



# SEHEMU SITA ANAZOWEZA KUTUA XAVI ANAPOONDOKA BARCELONA

**BARCELONA, Hispania**

ENZI ambayo iliwahi kuahidi mengi kule Barcelona imefikia kikomo chake.

Xavi Hernandez, kiungo wa kati ambaye aliwahi kuwa kitovu cha Wakatalunya walioshinda kila kitu chini ya Pep Guardiola, alifichua Januari kwamba muda wake kama kocha wa Barca utafikia tamati mapema mwishoni mwa msimu huu wa msimu wa 2023/24.

Msimu wa sasa umekuwa wa kutojali kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Hispania, huku mvutano unaoizunguka klabu hiyo ukichangia sana uamuzi wa Xavi kujiuzulu.

Mengi ya mazungumzo baada ya tangazo la Xavi yamelenga ni nani atamrithi Mhispania huyo kwenye usukani huo.

Lakini hapa 90min inaangalia sehemu sita ambazo Xavi anaweza kutua baada ya kuondoka Barcelona.

**#6. Liverpool**

Kama Barcelona, Liverpool watakuwa wakiwinda kocha mpya msimu wa majira ya joto baada ya Jurgen Klopp kufichua kwamba atajiuzulu mwishoni mwa msimu huu baada ya miaka tisa ya kukaa Anfield.

Lakini, Xavi si jina ambalo 'Wekundu' hao wanaweza kulifikiria sana. Kazi yake haipendekezi kuwa atakuwa na uwezo wa kuongoza klabu yenye hisia nyingi kupitia ambayo inaweza kuwa ujenzi chungu baada ya Klopp kuondoka.

Liverpool wana uwezekano mkubwa wa kumlenga mchezaji mwenzake wa zamani wa kimataifa wa Xavi, Xabi Alonso kwa nafasi hiyo badala yake.

**#5. Chelsea**

Chelsea wanatamani mradi wa Mauricio Pochettino kuwa mzuri kwa sababu nyingi. Hata hivyo, msimu wa kwanza wa Muargentina huyo umekuwa na taabu kwenye mbio za kuwania mafanikio yao katika mataji.

'The Blues' hao kwa mara nyingine tena wako katikati ya msimamo wa Ligi Kuu, na kuna uwezekano wa klabu hiyo kuachana na Pochettino iwapo kampeni yao itaisha sawa na 2022/23 (walimaliza nafasi ya 12 katika msimamo).

Ikiwa mmiliki Todd Boehly ataamua kuachana na kocha huyo, baada ya kushindwa tena, basi Xavi huenda likawa jina wanalozingatia. Hata hivyo, mashabiki wa Chelsea wana uwezekano mkubwa wa kutaka kurejeshwa kwa DNA iliyowafanya kufanikiwa sana chini ya umiliki wa Roman Abrahmovich.

Kwa hali ilivyo, ni vigumu kufikiria kumuona Xavi akivamia Uwanja wa Stamford Bridge.

**#4. Kurudi Qatar**

Xavi alimaliza muda wake wa kucheza nchini Qatar akiwa na Al Sadd kabla ya kuanza kazi yake ya ukocha katika klabu hiyo hiyo.

Mhispania huyo alifurahia mafanikio mengi nchini Qatar na pengine atakuwa tayari kurejea ikiwa angependa muda wa kutoonekana baada ya kustahimili changamoto hapo Katalunya.

Hata hivyo, kibarua cha timu ya taifa kina uwezekano mkubwa kuliko kurejea katika Ligi Kuu ya Qatar na Al Sadd. Kwa kudhani Xavi ni mtu mwenye malengo ya hali ya juu, ana nini cha kuthibitisha kwenye klabu ambako amekuwapo na kufanya hivyo?

Kiungo huyo wa zamani aliwahi kusema kuwa atakuwa tayari kufundisha Timu ya Taifa ya Qatar kwenye Kombe la Dunia la 2022, na sasa anaweza kutamani kuwaongoza katika safari yao ya kuelekea kwenye mashindano ya 2026.

**#3. Timu ya Taifa ya Hispania**

Xavi alipata mafanikio ambayo hayajawahi kushuhudiwa akiwa na Timu ya Taifa ya Hispania walipotwaa mataji matatu mfululizo ya mashindano makubwa kati ya 2008 na 2012, na kushinda Kombe lao la Dunia la kwanza mwaka 2010.

Luis de la Fuente anakabiliwa na mtihani mkubwa msimu huu wa Euro 2024, huku kocha huyo wa Hispania asiyejulikana akichukua nafasi ya Luis Enrique baada ya Kombe la Dunia la 2022.

Ingawa amefanya kazi nzuri hadi sasa, msimamo wa chini chini wa De la Fuente unafanya nafasi yake kuwa hatarini. Shirikisho la Soka la Hispania lina nia ya kuongeza mkataba wa kocha huyo hadi Kombe la Dunia la 2026, lakini wengi watakuwa wakitaka kumkata kichwa chake endapo Hispania haitakuwa na mafanikio kule Ujerumani.

Kwa kuzingatia hadhi ya Xavi na upatikanaji wake, ni jina ambalo Hispania litalizingatia ikiwa watafikiria kuachana na Fuente. Hali ya kutohitaji sana kwa kalenda ya kimataifa inaweza pia kumfaa bosi huo wa Barcelona.

**#2. Sevilla**

Kuendelea kuzunguka Hispania kunawezekana kwa Xavi. Hata hivyo, kocha huyo wa Barcelona hatarajiwi kupata kibarua kikuu cha LaLiga.

Klabu mbili za Madrid vimetoka kwenye jedwali, Ernesto Valverde anatamba akiwa na Athletic Club, Imanol amechukuliwa na Real Sociedad, huku Valencia wakijipanga na nguli wa klabu hiyo, Ruben Baraja kushika usukani.

Bado, kuna chaguzi kadhaa za Xavi. Washindani wa taji Girona wanaweza kuwa macho wakati wa majira ya joto kutokana na nia inayoendelea kwa Michel, na Real Betis inaweza kuachana na Manuel Pellegrini. Hata hivyo, ni hakika kwamba nafasi itafunguliwa Sevilla na hii inaweza kuwa njia bora ya Xavi kusalia LaLiga.

Sevilla wamekuwa wasumbufu kwa miaka kadhaa, licha ya mafanikio yao ya Ligi ya Europa msimu uliopita. Kocha Quique Sanchez Flores kwa sasa anapambana kuiongoza klabu hiyo ya kihistoria kujiepusha na kushuka daraja.

Flores ni suluhu ya muda mfupi ambaye kwa hakika hatakuwa kwenye klabu hiyo mwanzoni mwa 2024/25. Ni kazi ngumu kutokana na muundo wa kikosi, lakini ambayo Xavi anaweza kutamani kuichukua.

**#1. Ligi Kuu ya Saudia**

Sio tu kipaji cha uchezaji Ulaya ambapo Saudi Arabia inajaribu kuwinda. Ufalme pia umejaribu kuwazawadia baadhi ya akili bora zaidi za kufundisha mchezo.

Jose Mourinho na Massimiliano Allegri ni miongoni mwa makocha waliopokea ofa nono kutoka kwa Saudia, huku magwiji kama Jorge Jesus na Marcelo Gallardo wakiwa miongoni mwa wanaofundisha huko kwa sasa.

Xavi ni jina la nyota ambalo bila shaka litawavutia wale walio katika Ufalme wenye fedha, huku uzoefu wa Mhispania huyo wa Mashariki ya Kati ukitoa chaguo hili kwa uwezekano zaidi kuliko njia mbadala za Ulaya. Kocha huyo wa Barcelona hivi majuzi alionyesha kuvutiwa kwake na mradi wa SPL, akisema waziwazi Januari: "Mimi ni shabiki mkubwa wa Ligi ya Saudia."



XAVI

## Nukuu


"Unaendelea kuniuliza kuhusu mchezaji anayechezea timu nyingine. Tayari tuna wachezaji bora zaidi duniani hapa. Kwa mpangilio: Vini Jr wa kwanza, Bellingham wa pili, Rodrygo wa tatu. Kisha Kroos, Valverde, Camavinga," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, alipoulizwa endapo Kylian Mbappe, atajiunga na klabu hiyo msimu ujao.**



"Mimi ni mtu ambaye hubadilika na kucheza nafasi nyingi inapohitajika. Najua nitafanya hivyo nikiwa na Manchester City na lazima niwe tayari. Ninafurahia kucheza katikati na hapo ndipo ninapojiona. Natumai naweza kupata muda zaidi wa kucheza hapo," **Kiungo wa kati wa Manchester City, Phil Foden**




"[Jurgen] Klopp ni kocha mzuri, lakini sidhani kama huu ni wakati wa kuzungumza juu yake. Kocha mpya atataka kufanya mabadiliko, lakini kwanza itabidi tumweleze mradi na mawazo. Kocha mpya anatakiwa kufuata mstari wa kazi. Kamwe hatutakuwa timu ambayo haitaki kucheza vizuri, ambayo haitaki kuwa na mpira. Kuanzia kwenye wazo hilo, kila kocha ana sifa zake, lakini yeyote anayekuja lazima awe na njaa ya kufanya mambo makubwa," **Mkurugenzi wa Michezo wa Barcelona, Deco.**



Nipashe
Spotika



# USAJILI WA DIRISHA DOGO ULIOANZA KULIPA LIGI KUU




Straika mpya wa Simba, Pa Omar Jobe (kulia mwenye rasta), akipongezwa na wachezaji wenzake, Saido Ntibazonkiza na Sadio Kanoute baada ya kupachika bao la kwanza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Tabora United, Jumanne iliyopita kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora.

**Na Adam Fungamwango**

UHAMISHO wa wachezaji kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara ulifunguliwa Desemba 26 na kufungwa Januari 15, moja kwa moja wachezaji wapya wakaanza kuingia mzigoni.

Kuna wachezaji wanaotoka nje ya nchi, wakicheza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu Bara, wengine ni wa hapa hapa wakihama tu timu moja kwenda nyingine.

Ingawa wamesajiliwa wengi, lakini baadhi yao wameshaanza kuonyesha ni kwa nini wamesajiliwa. Wameingia kwenye klabu zao mpya na kuonyesha kwa nini walisajiliwa, kwa kuongeza kitu.

Baadhi tayari wameshaanza kupachika mabao, wengine walionekana kuongeza nguvu kwenye vikosi na kuonekana kuwa imara, tofauti na mwanzo.

Katika makala haya tunawachambua baadhi ya wachezaji ambao muda mfupi tu baada ya kujiunga na timu zao, tayari wameshaanza kufanya mambo.

**1# Mohamed Mustapha - (Azam FC)**

Amesajiliwa kwenye dirisha dogo kwa ajili ya kuziba pengo la makipa mawili majeruhi, Mcomoro, Ali Ahamada na Mghana Iddrisu Abdulai.

Alikuwa kwenye kiwango cha juu Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa CCM Kirumba wakati timu yake ilipocheza dhidi ya Simba, mechi ikiisha kwa sare ya bao 1-1.

Aliokoa hatari nyingi na kuonekana mhimili mkubwa kwenye kikosi cha Azam katika kuinyima Simba ushindi.

Na siyo kama alibahatisha kwani anakumbukwa kuwa alifanya kazi nzuri wakati akicheza kwenye klabu yake ya Al Merrikh Omdurman ya Sudan ilipocheza dhidi ya Yanga katika michezo miwili wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Pamoja na kwamba Yanga ilifanikiwa kusonga mbele, lakini uwezo wake ukawasukuma Azam FC kumsaka kipa huyo.

Yupo Azam kwa mkopo wa miezi sita na kama akiendelea hivi, kuna uwezekano mkubwa akabakia msimu ujao na kutengeneza safari ya makipa wengine waliobaki.

**2# Babacar Sarr - (Simba)**

Awali hata mashabiki wa Simba walikuwa bado hawajamuelewa kiungo huyo mkabaji aliyesajiliwa kutoka US Monastir ya Tunisia. Lakini kila mechi anayocheza baadaye anakuwa bora kuliko iliyopita.

Kwa sasa mashabiki wengi wa Simba wameonekana kukubali uwezo wake kwa jinsi anavyoituliza timu na kujua kukaa kwenye maeneo ya kati wakati timu inaposhambuliwa.

Kwa kiasi kikubwa wametibu udhaifu wa Simba kukatika kati na kuonekana hakuna mtu yeyote hasa inaposhambuliwa.

**3# Emmanuel Mtumbuka-(Mashujaa FC)**

Alifunga bao la kuwasazisha katika mechi ya Alhamisi iliyopita wakati timu yake ya Mashujaa FC ikicheza dhidi ya Yanga katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Wakati Yanga ikiongoza kwa bao moja lililofungwa na Maxi Nzengeli, Mtumbuka alisawazisha kabla ya Mudathir Yahaya kufunga bao la pili dakika nne kabla ya mechi kumalizika.

Ni matunda ya usajili wa dirisha dogo, kwani Mashujaa ilimsajili kutoka Stand United inayocheza Ligi ya Championship kwa sasa.

**4# Pa Omar Jobe-(Simba**

Ni straika mpya wa Simba aliyesajiliwa kwenye uhamisho wa dirisha dogo akitokea Klabu ya FC Zhenis inayoshiriki Ligi Kuu nchini Kazakhstan.

Ameifungia Simba mabao mawili katika mechi nne alizocheza, akiwa na bao moja kwenye Ligi Kuu katika michezo mitatu ambayo tayari amekipiga.

Alifunga bao lake la kwanza Januari 31 katika mechi ya Kombe la FA dhidi ya Tembo FC, Simba ikishinda mabao 4-0, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Amecheza mechi tatu za Ligi Kuu ingawa si kwa dakika zote 90, bali alikuwa akibadilishana na mwenzake Freddy Michael.

Alifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu katika mechi dhidi ya Tabora United na aliisaidia Simba kusawazisha bao katika mechi dhidi ya Azam FC.

Ni yeye ndiye alifanyiwa madhambi yaliyosababisha faulo iliyozaa bao katika dakika za majeruhi akiwa ameingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Freddy.

**5# Yeison Fuentes - (Azam FC)**

Pamoja na kwamba Azam imesajili wachezaji wawili kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo, lakini aliyeonekana kukubalika kwa mashabiki wa soka ni beki wa kati, Yeison Fuentes raia wa Colombia aliyesajiliwa kutoka Klabu ya Leones FC ya kwao.

Katika mechi yake ya kwanza tu ya Ligi Kuu dhidi ya Simba alionekana kama anaifahamu vema Ligi ya Tanzania, hakuonekana kama mgeni.

Aliweka ulinzi madhubuti akisaidiana na Yannick Bangala ambaye alicheza namba nne katika mechi iliyoisha kwa sare ya bao 1-1.

6# Freddy Michael - (Simba)

Licha ya kwanza anaonekana bado hajawa kwenye kiwango ambacho mashabiki wanakihitaji huku akionekana bado hajachangamka, hajawa msumbufu kwa mabeki kama mwenzake Pa Jobe, lakini takwimu zinambeba.

Katika mechi nne ambazo amecheza tangu asajiliwe Simba, tayari ana bao moja na 'asisti' juu, tatu zikiwa za Ligi Kuu.

Katika mechi ya Ligi Kuu iliyochezwa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi dhidi ya Tabora United, Jumanne iliyopita, alifunga bao moja likiwa la nne katika mchezo huo.

Asisti yake ilikuwa kwenye Kombe la FA, wakati Simba ilipoisulubu Tembo FC, mabao 4-0, Januari 31, Azam Complex, Dar es Salaam.

**JE, WAJUA?**




MABAO mawili aliyofunga Jude Bellingham juzi wakati Real Madrid ikishinda 4-0 dhidi ya Girona, yanamfanya kuwa mchezaji wa nafasi ya kiungo aliyefunga mabao mengi zaidi katika historia ya klabu hiyo kwenye La Liga kwa msimu mmoja katika karne hii. Pia ni mchezaji wa kwanza wa Real Madrid kufunga katika kila mechi nne za kwanza za Ligi ya Mabingwa kwa klabu hiyo - na anasalia kuwa mfungaji bora wa La Liga msimu huu akiwa na mabao 16.





## Manyoni yajivunia kukusanya bil.18/-

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida imekusanya kiasi cha Sh.bilioni 18 sawa na asilimia 62 ya makadirio ya Sh. bilioni 29 hadi kufikia Januari 2024 katika vyanzo mbalimbali vya mpato kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Jumanne Mlagaza, akizungumza juzi wakati akifungua kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo, alisema kati ya fedha hizo Sh. bilioni 1.8 zimekusanywa kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani.

Alisema katika kipindi hicho halmashauri hiyo imepokea Sh.bilioni 5.8 kutoka serikali kuu na wafadhili ambazo zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika ngazi ya kata na vijiji.

Mlagaza aliwataka wataalamu na viongozi kila mmoja atimize wajibu wake kikamilifu kwa kushirikiana na madiwani katika kusimamia miradi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato pamoja na usimamizi wa fedha kwa ustawi wa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na taifa kwa ujumla.

"Madiwani na watendaji tuna jukumu la kusimamia fedha zinazoletwa na serikali kwenye halmashauri yetu ili ziweze kutumika kwa malengo yaliyokusudia, nisisitize upendo miongoni mwa madiwani na watendaji na tujenge utamaduni wa kushuka chini kusikiliza kero za wananchi," alisema Mlagaza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Jimson Mhagama, alisema kila mtendaji atimize wajibu wake katika eneo lake na kwamba ikitokea kuna tatizo atawajibike yeye kama yeye na si vinginevyo.

Kuhusu fedha zaidi ya Sh.bilioni 1.4 zilizoletwa na serikali kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya Wilaya, alisema haziwezi kubadilishwa matumizi na kwamba wanaotaka fedha hizo zipelekwe kwenda kuanzisha ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya hilo kamwe haliwezi kutekelezwa.

"Kama tunataka kujenga hospitali mpya ya wilaya, hivi karibuni tutaanza vikao vya bajeti tuweke suala hili kwenye bajeti ijayo kwamba tunaomba Sh.bilioni 2 au 3 kuanza ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya lakini sio hizi fedha zilizoletwa ndo tuzichukue kwenda kuanzisha ujenzi hilo halitekelezeki," alisema.

Mhagama alisema yapo maneno kwamba baadhi ya majengo katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni ambayo yamechakaa halmashauri inataka kuyabomoa jambo ambalo si la kweli.

Hatua ya Mkurugenzi huyo kutoa ufafanuzi huo ilitokana na madai ya baadhi ya madiwani kutaka fedha zilizoletwa na serikali kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya hospitali ya wilaya zibadilishwe matumizi.

# Bashungwa atoa mwezi kamati kukamilisha kazi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, ametoa mwezi mmoja kwa kamati inayoandaa mkakati wa kuongeza ushiriki makandarasi wazawa kwenye miradi mbalimbali nchini kukamilisha maboresho yatakayowezesha kampuni ya wazawa kupata miradi ya ujenzi na fedha nyingi kubaki nchini.

Bashungwa alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki jijini hapa, wakati wa kikao kazi cha uwasilishaji wa taarifa hiyo na kusisitiza kamati kuangalia maeneo muhimu ikiwamo uandaaji wa nyaraka za zabuni, vigezo vya upataji wa miradi, mikataba na masuala ya kisheria.

Alisema umuhimu wa ushirikishwaji wa wazawa katika nchi kutasaidia fedha nyingi kubaki nchini na kukuza biashara za wazawa, kuongeza ajira na ujuzi kwa wataalamu wa ndani, kupunguza matumizi ya fedha za kigeni, kujenga kampuni ya ndani kuwa makubwa na yenye uwezo wa kushindana kimataifa.

"Fanyeni utafiti kuona nchi nyingine zimefanikiwa vipi katika suala la kuwajengea uwezo wataalam wao (Local Content), hakikisheni ripoti ya mwisho inafikisha matarajio yote ya wataalamu wa sekta ya ujenzi," alisema Bashungwa.

Aidha, Bashungwa alisisitiza umuhimu wa mkakati huo katika kuongeza wigo wa kuwajengea uwezo wataalam wa sekta ya ujenzi nchini ili kuhakikisha utalaam na ujuzi unakuzwa kwa maendeleo ya nchi.

Alisema taarifa hiyo pia iweke mazingira wezeshi ya kusaidia makandarasi wazawa kutekeleza miradi kwa kuwa serikali imeweka kwenye sheria kiwango cha thamani ya miradi iliyokuwa ikitekelezwa na wazawa kutoka Sh. bilioni 10 hadi bilioni 50 ili kuwawezesha wazawa kunufaika na miradi hiyo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Matiko Mturi ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), alimwahakikishia waziri huyo kuwa kwa kushirikiana na wadau wote wataendelea kukusanya maoni, ili mkakati huo uwe na manufaa kwa pande zote na usaidie katika kukuza uchumi wa nchi.

Alisema kuwa miradi ya ujenzi iliyotekelezwa katika kipindi cha miaka 10 kuanzia Januari 2013 hadi Juni 2023 ni 36,839 yenye thamani ya Sh. trilioni 61.6 ambayo ilisajiliwa.

Kamati ya uaandaji wa Mkakati wa Ushiriki wa Wazawa katika miradi ya ujenzi imehusisha Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB), Bodi ya Usajili ya Makandarasi (CRB), Bodi ya Usajili ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).



Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Tabora, Hawa Mwaifunga, akisisitiza jambo baada ya wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), walipotembelea jana mashamba ya korosho wilayani Manyoni mkoani Singida kukagua maendeleo ya mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha mashamba ya korosho. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mchengerwa awataka kujifunza kwa Halmashauri ya Kwimba

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ametoa wito kwa halmashauri zote nchini kuiga mfano wa Halmashauri ya Kwimba iliyoibuka kinara katika matumizi sahihi ya mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma (NeST).

Mchengerwa, aliyasema hayo jana jijini Dodoma akiwa wakati wa hafla ya utoaji tuzo hiyo iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma PPRA kupitia Mkurugenzi wake Mkuu, Eliakim Maswi.

Alisema, hatua hiyo ni ishara ya weledi wa taasisi za umma katika kutii agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, katika kuhakikisha serikali inatekeleza majukumu yake kiutendaji kupitia mifumo, ili kuleta ufanisi wa kazi sambamba na kupunguza gharama za matumizi na hatimaye kuokoa fedha za umma.

"Nadhani tumeweza kumsikiliza mkurugenzi hapa akieleza ni kwa namna gani kupitia mfumo huu wameweza kupunguza gharama za matumizi, suala ambalo limeweza kuisaidia serikali kuokoa fedha ambazo pengine zingetumika ndivyo sivyo" alisema Mchengerwa.

Mkurugenzi Mkuu wa PPRA, Eliakim Maswi, alieleza kufurahishwa na utendaji kazi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kwimba.

"Mheshimiwa Waziri unajua ilipo Halmashauri ya Kwimba ni pembeni, lakini pamoja na kuwa pembeni alichokifanya Mkurugenzi wa Kwimba sisi kama mamlaka tumefurahishwa sana na utendaji wake tukaona tuje kumsema mbele yako kuwa huyu mkurugenzi anatufanyia kazi nzuri bila kulalamika kuwa mfumo unamsumbua," alisema Maswi. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kwimba, Happiness Msanga, alisema siri ya mafanikio hayo waliyoyapata kwa kipindi hiki kifupi tangu kuanzishwa kwa mfumo wa NeST ni pamoja na kujizatiti katika ufanya kazi kwa kutoa elimu ya kutosha kwa watumishi wote.

Alisema elimu hiyo ilijumuisha uwezeshaji wa mkuu wa wilaya, wajumbe wa kamati ya usalama, katibu wa chama sambamba na watumishi wa makundi wakiwamo walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari, wakuu wa vituo vya afya na zahanati pamoja na watendaji wa kata na vijiji.

Alisema njia nyingine ni kutoa msaada wa kufanya maombi ya tenda kwa wazabuni wasiokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya mfumo wa NeST kwa kuwapa msaada kupitia watu wa ununuzi sambamba na wataalamu wa TEHAMA.

Kadhalika, alisema kupitia Mfumo wa NeST umewasaidia sana kwenye mambo mengi ya ununuzi, ikiwa ni pamoja na kushuka kwa gharama za bidhaa na kupunguza migogoro na lawama za upatikanaji wa tenda.

"Sasa hivi kupitia mfumo hakuna mtumishi anayekuja kulalamika kuwa mtu wake hajapata tenda wala mfanyabiashara kutokana uwepo wa uwazi kwenye mfumo, maana kupitia mfumo sasa hata mzabuni ambaye hajashinda ataona sababu ya kwanini hakushinda na aliyeshinda ataona sababu iliyompelekea kushinda," alimalizia. Halmashauri ya Kwimba imejinyakulia tuzo hiyo ya kiasi cha Sh. milioni 10 kwa kuwa taasisi ya umma kinara katika matumizi ya mfumo wa NeST katika kufanya ununuzi kufuatia kutangaza zabuni nyingi zaidi kuliko taasisi nunuzi yoyote serikalini.

Jumla ya zabuni ilizotangaza mpaka sasa ni 472 ikifuatiwa na Halmashauri ya Ngara iliyotangaza zabuni 150 sambamba na Halmashauri ya Mbarali ambayo imetangaza zabuni 141.



# Walimu 17 matatani kutoza michango ya madawati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WALIMU 17 wa shule za msingi na sekondari jijini Mbeya, wamechukuliwa hatua za kinidhamu kwa tuhuma za kukiuka miongozo ya serikali kwa kuwachangisha wanafunzi madawati, ili wawaandikishe kuanza shule.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa aliyasema hayo juzi kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya wilaya hiyo ambapo alisema kati ya walimu hao wanane ni wa shule za msingi na tisa ni wa shule za sekondari za jiji hilo.

Malisa alisema walimu wa shule za msingi wamechukuliwa hatua katika ngazi ya wilaya na wale wa sekondari yamepelekwa mapendekezo katika ngazi ya mkoa ambako ndiko kwenye mamlaka ya kuwashughulikia.

Alisema serikali ilishaondoa michango yote isiyokuwa ya lazima kwenye shule zake zote na hivyo kitendo walichokuwa wanakifanya walimu hao kilikuwa kinakinzana na maagizo hayo ya serikali.

"Hakuna mwanafunzi anayepaswa kuchangishwa dawati anapokwenda shuleni, sasa hawa walimu walikuwa wanaendeleza utaratibu huo ambao unawanyima fursa ya kusoma baadhi ya watoto hasa wanaotoka kwenye familia maskini, kwa hiyo tumeshawachukulia hatua," alisema Malisa.

Mchumi wa Jiji la Mbeya, Ally Nunduma alisema halmashauri hiyo ina mikakati mbalimbali ya kumaliza tatizo la upungufu wa madawati katika shule zote za sekondari na msingi kwa kutumia mapato ya ndani.

Alisema walifanya ufuatiliaji katika shule zote na kubaini kuwa wanafunzi 806 na hivyo wakaamua kuanza utengenezaji wa madawati kwa kutumia mapato ya ndani na kuyasambaza kwenye shule zenye upungufu kwa awamu.

Alisema awali jukumu la kutengeneza madawati hayo lilikuwa linatekelezwa na madiwani pamoja na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, lakini kwa sasa linatekelezwa na halmashauri yenyewe kwa kutumia mapato ya ndani.

"Madawati mengine yanatengenezwa na Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) na mengine yanatengenezwa na mafundi jamii wetu, kila yanapokamilika tunayachukua na kuyapeleka kwenye shule zetu na lengo letu ni kuhakikisha tatizo la upungufu wa madawati linafikia mwisho," alisema Nunduma.

Baadhi ya wadau walioshiriki kikao hicho walishauri serikali kuendele kusimamia nidhamu na maadili ya watumishi, ili kukuza kiwango cha elimu katika shule mbalimbali.

Katibu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Alunas Gift, alisema mbali na kuwachukulia hatua walimu hao pia kuna tatizo la walimu kuwataka wanafunzi kwenda kufanya mitihani kila Jumamosi na kuwachangisha Sh. 1,000 kila mmoja.

Alisema michango hiyo pia imekuwa kero kwa wazazi akieleza kuwa michango hio huwa ni ya lazima na kwamba mwanafunzi asiyekuwa na hela haruhusiwi kufanya mitihani hiyo na anarudishwa nyumbani.

Vilevile, aliomba serikali kudhibiti vituo vya nje vya masomo ya ziada (Tuition centers) akieleza kuwa vimekuwa vikichangia kuharibu maadili ya wanafunzi.

Alisema wamiliki wa vituo hivyo wamekuwa wakivitumia vituo hivyo kama biashara bila kuzingatia malezi sahihi ya watoto kama ilivyo kwenye shule za kawaida.



Baadhi ya vijana wanaoopoa mchanga kwenye Mto Mbalizi uliopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, wakipakia mchanga kwenye gari jana asubuhi, shughuli hiyo imekuwa ikilalamikiwa kuwa inachangia uharibifu wa mazingira kwenye mto huo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Watu 11 wafariki dunia kwa mafuriko Mbarali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WATU 11 wamefariki kwa kusombwa na mafuriko na kuangukiwa na nyumba kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya katika kipindi cha miezi mitatu ambayo mvua imenyesha wilayani humo.

Aidha, mafuriko hayo yanadaiwa kuharibu miundombinu hasa barabara na kusababisha baadhi ya maeneo kutofikika yakiwamo maeneo ya mashamba hali iliyozidi kuhatarisha maisha na uchumi wa wananchi wa maeneo hayo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mbarali, Twalib Lubandamo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu madhara ya mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Alisema taarifa zilizokusanywa katika ofisi ya mkuu wa wilaya hiyo zinaonyesha mvua hiyo imesababisha madhara kwa binadamu hasa vifo na uharibifu wa makazi.

Alisema moja kati ya watu waliofariki kutokana na mafuriko hayo ni mwanafunzi ambaye hata hivyo hakumtaja kwa jina na kwamba alikuwa mkazi wa Kata ya Utengule Usangu ambaye alisombwa na maji.

"Taarifa za maafa haya ni za maeneo tofauti sasa kata ya Chimala na Utengule Usangu, ambako asilimia kubwa mifereji imekatika na mazi kusambaa ovyo, lakini baadhi ya nyumba zilianguka kutokana na mvua iliyokuwa imeambatana na upepo mkali," alisema Lubandamo.

Alisema barabara nyingi za wilaya hiyo zimeharibika na hazipitiki na kwamba kutokana na mazingira ya wilaya hiyo miundombinu hiyo haiwezi kutengenezeka kwa sasa mpaka mvua itakapokuwa imepungua ama kuisha.

Lubandamo alisema barabara zote zilizoharibika ni zile zilizojengwa kwa kiwango cha changarawe kwa maelezo kuwa hakuna barabara iliyojengwa kwa kiwango cha lami ambayo imeharibika.

# Pori la Mpanga Kipengere latajwa kuwa kivutio kikubwa

**Na Elizabeth John,** MAKETE

PORI la Akiba la Mpanga Kipengere lililopo katika mikoa ya Njombe na Mbeya limetajwa kuwa moja ya vivutio vya watalii vinavyovutia katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kutokana na uwepo wa maporomoko mengi ya maji na uoto wa asili.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda baada ya kufanya ziara ya kutembelea pori hilo kwa lengo la kuangalia utunzaji wa mazingira hasa vyanzo vya maji.

"Eneo hili ni la kipekee sana, maporomoko jinsi yalivyopangika ngazi ukiziangalia unashangaa uumbaji wa Mungu ulikuwaje katika eneo hili, lakini kitu kingine cha ajabu sana ukifika kwenye maporomoko yale kuna mvuke wa ajabu sana utafikiri kuna AC," alisema Sweda.

Aliwahamasisha wataalamu pamoja na wananchi wa wilaya hiyo kwamba wanapokuwa wamechoka waende mpanga kipengere kwa ajili ya kupumzika.

"Siku tukiwa tumechoka sana tuje mpanga Kipengere sio tumechoka tu tunataka tunataka kupumzisha akili ili zitulie, ubongo utulie majibu ni mpanga Kipengere hakuna sehemu nyingine," alisema Sweda.

Mkuu wa Hifadhi ya Mpanga Kipengere, Donasian Makoi, alisema lengo la kuanzishwa kwa pori hilo ni kwa ajili ya uhifadhi wa vyanzo vya maji, wanyamapori na mimea.

"Huko ndani pia kuna mimea adimu kweli kweli na viumbe mbalimbali ambavyo vinafanya maisha ya viumbe wengine waendelee kuwepo, lakini lengo la maji ni kwamba vyanzo vingi vya maji ambavyo vinalisha Mto Ruaha Mkuu vinatokea ndani ya Pori ya Mpanga Kipengere, lakini Mto Ruaha Mkuu ndiyo unalisha haya mabwawa ya kuzalisha umeme La Kidatu, Mtera na bwawa jipya la sasa la Mwalimu Nyerere," alisema.

Makoi alisema hivi sasa dunia inakabiliwa na mabadiliko ya tabia nchi jambo ambalo limesababisha ukosefu wa mvua za kutosha na maeneo mengi kupata ukame na majanga mbalimbali.

"Kwa hiyo serikali kuwa na umakini mkubwa kupitia wilaya kuhakikisha eneo kama hili nyeti kwenye uhifadhi wa vyanzo vya maji linaendelea kuwepo, lakini kwenye eneo hili kiutalii kwa nyanda za juu kusini ni eneo la kipekee," alisema Makoi.

Alisema Pori la Akiba la Mpanga Kipengere ni hifadhi yenye maporomoko mengi ambayo ndiyo kivutio kikubwa.

"Sisi kama hifadhi tunaendelea kuhamasisha utalii wa ndani kueneleza juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kupitia makala au filamu ya 'The Rolay Tour' ambayo inahamasisha utalii wa ndani lakini pia watalii wa nje," alisema Makoi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe, alisema eneo la Pori la Mpanga Kipengere ni eneo linalojumuisha maporomoko ya maji pamoja na bustani za maua ya asili.

"Sasa ni eneo ambalo serikali imewekeza sana, ni eneo ambalo watu wanaweza kuja kupumzika na kuona namna ambayo kuna mandhari mazuri, miundombinu mizuri, uasili uliopo hapa, maji, maporomoko, maua, milima na misitu mpaka wanyama wapo katika hifadhi hii," alisema Makufwe.

Aliongeza kuwa, "Pia kuna bwawa la kuogelea la asili, maji masafi, maji mazuri yanayotiririka yasiyochafuka, yale mengine mtu anaogelea hapa na mwingine hapa mnatumia maji hayo hayo sasa ukija mpanga kipengere unakutana na maji yanayotiririka yakiwa safi kabisa maji mazuri," alisema Makufwe.

Hata hivyo, Makufwe aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi ili kufika katika hifadhi ya mpanga Kipengere ili kujionea mandhari nzuri kwa ajili ya kufanya utalii wa ndani.





# Msajili wa Hazina ateta na watendaji wa taasisi

**Na Mwandishi Wetu**

MSAJILI wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waheed Ibrahim Sanya, amewataka watendaji wa taasisi na mashirika ya umma kushirikiana na ofisi hiyo ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi.

Akifungua mkutano wa kuwajengea uelewa watendaji wakuu wa taasisi za uwekezaji wa umma visiwani humo, alisema jana kuwa kikao hicho kitawawezesha kufahamu majukumu yao pamoja na kujua Ofisi ya Msajili wa Hazina na nafasi yake kiutendaji.

Alisema Hazina ni taasisi kubwa inayofanya kazi kwa karibu na taasisi nyingi za serikali hasa zinazozalisha, hivyo ni wajibu wao kufanya kazi kwa bidii ili kuleta maendeleo nchini.

Alisema lengo la mkutano huo ni kujenga uelewa kwa watendaji wa taasisi hizo juu ya kazi zinazofanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na kuwapatia fursa ya kuwasilisha changamoto zinazowakabili katika taasisi zao na kuzipatia ufumbuzi.

Alisema ofisi hiyo ina mpango wa kuwapatia mafunzo ya mwongozo kwa baadhi ya watendaji ili kuwajengea uwezo na kuleta mabadiliko chanya katika taasisi zao.

"Watendaji wakuu wa taasisi hizi watakuwa na uelewa mzuri juu ya ofisi hii, watatekeleza majukumu yao ipasavyo na kuwa mabalozi wazuri kwa wanaoowaongoza," alisema Sanya.

Akiwasilisha mada ya uhusiano baina ya ofisi na mashirika ya umma na mpangokazi wa ofisi hiyo, Kaimu Mkuu wa Mashirika ya Uwekezaji ya Umma, Mussa Ali Juma, alisema serikali inatoa gawio kwa taasisi zake kupitia uchangiaji wa taasisi hizo ili kuendeleza utendaji kazi wao na kuleta maslahi kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Mussa alisema kuwa kuna haja ya kuwa na mwongozo mmoja katika taasisi kutokana ma kuwapo miundo tofauti katika taasisi hizo.

Alisema lengo ni kuona taasisi hizo zinafanya uwekezaji mzuri kwa maslahi ya taifa na wao ndio wenye jukumu la kutoa mwongozo na kusimamia mali za umma katika taasisi hizo.

Alisema kuwa kazi yake kubwa ni kuruhusu kutumia au kuondolewa kwa mali za umma pamoja na kutoa mwongozo utakaoelekeza namna nzuri ya kuongoza taasisi zao.

Washiriki wa mkutano huo waliahidi kutoa ushirikiano wao kwa ofisi hiyo.

Mkutano huo umeshirikisha taasisi mbalimbali za kibiashara ikiwamo Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC), Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Shirika la Uvuvi Zanzibar (ZAFICO), Shirika la Magazeti, Shirika la Utangazaji na Shirika la Bandari.

# Dk. Mwinyi aahidi kuimarisha matibabu ya moyo Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali yake iko tayari kukuza ushirikiano na kutunza rasilimali ili kuendeleza juhudi za utafiti, kinga, matibabu ya moyo na mishipa ya damu.

Amesema ushirikiano huo utaleta mabadiliko makubwa katika kuboresha matokeo ya athari ya magonjwa ya moyo kwa kila mmoja visiwani humo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi visiwani humo wakati akifunga mkutano wa wataalamu wa magonjwa ya moyo Afrika ulioandaliwa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

"Kwa madhumuni ya kuboresha huduma za mfumo wa moyo na mishipa ya damu, Serikali ya Zanzibar itashirikiana na JKCI na taasisi zingine duniani na ushirikiano huu utahakikisha wagonjwa wa Zanzibar wanaogundulika kuwa na magonjwa hayo wanapata huduma na matibabu ya dharura kwa wakati ili kupambana na vifo vinavyoweza kuepukika," alisema.

Dk. Mwinyi aliagiza Wizara ya Afya Zanzibar kuanza majadiliano na JKCI ili huduma za upasuaji na matibabu ya moyo zianze kutolewa Zanzibar.

Alisema hatua hiyo itasaidia kujenga uwezo kwa madaktari wazalendo wa Zanzibar na kupunguza gharama za matibabu, hivyo kuimarisha huduma za afya.

Alisema kuwa miongoni mwa vipaumbele vya serikali ni kuimarisha huduma za afya katika ngazi zote, hivyo uamuzi wa taasisi hiyo kutaka kuanzisha huduma za matibabu ya moyo katika Hospitali ya Mkoa (Lumumba) utachochea kufikwa kwa azma hiyo.

Alipongeza uamuzi wa JKCI kuitisha mkutano huo Zanzibar. Maarifa na utaalamu uliotolewa na madaktari bingwa na wabobezi utasaidia kuimarisha huduma za afya na kupunguza maradhi ya moyo kama vile kuziba kwa mishipa ya damu na mengineyo.

Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya JKCI, Asha Ressa, alisema kuwa kwa mwaka 2023, taasisi hiyo ilifanya uchunguzi wa magonjwa ya moyo katika mikoa zaidi ya 10 ikiwamo ya Zanzibar ambapo takriban watu 2,000 walichunguzwa.

"Katika kambi hizo, wapo wagonjwa waliopatiwa matibabu ya awali na waliokutwa na shida kubwa walipewa rufani, jambo lililookoa maisha, pia gharama za matibabu," alisema mwenyekiti huyo.

Akitoa maelezo kuhusiana na mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, aliomba Serikali ya Zanzibar kuridhia taasisi hiyo kufungua kituo cha matibabu ya moyo kwa wagonjwa wanaotokea Zanzibar na kuhudumiwa na taasisi hiyo.

Alisema JKCI inapokea zaidi ya wagonjwa 4,000 kwa mwaka ambao matibabu yao hudhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kwamba kufungua kituo cha matibabu visiwani humo kutapunguza gharama za matibabu, pia kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani.

Aliongeza kuwa mkutano huo umekuwa jukwaa muhimu la wataalamu wa magonjwa ya moyo kujifunza mambo mbalimbali yakiwamo matumizi ya teknolojia katika matibabu ya moyo, njia za upasuaji na kuunganika kwa wataalamu wabobezi na wa kawaida wa ngazi zote.

Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Khamis Hafidh, alisema mbali na uwekezaji uliofanywa na serikali kwa kujenga majengo ya kutolea huduma, vifaa na kusomesha wataalamu, pia inashirikiana na sekta binafsi katika huduma za dawa na vipimo ili kuongeza upatikanaji huduma bora za afya nchini.

Alisema serikali ilianzisha mfumo wa rufani za matibabu kuanzia katika ngazi ya afya ya msingi, wilaya, mkoa hadi taifa na kwamba utakapokamilika ujenzi wa Hospitali ya Binguni, utawezesha kupatikana huduma za kibingwa na kukamilika kwa mfumo wa utoaji huduma.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdallah (kushoto), akimkaribisha kwenye chama Mbunge wa zamani wa Viti Maalum CUF, Sonia Magogo, baada ya kutangaza kukihama chama chake na kuhamia CCM kufuatia kukoshwa na uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan katika mkutano uliofanyika viwanja vya Chanika, wilayani Handeni, mkoani Tanga. Kulia ni Mbunge wa Handeni Mjini, Reubine Kwagilwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi wapewa elimu ya kukabiliana na majanga

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Utumishi na Uendeshaji Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Khamisuu Hamid Moh'd, ameelekeza wafanyakazi walioshiriki mafunzo ya kukabilina na maafa kutumia vyema mafunzo hayo ili kuepusha athari za majanga yanayotokea katika sehemu za kazi.

Khamisuu alielekeza hayo jana wakati akifunga mafunzo yaliyotolewa na watendaji kutoka Kamisheni ya kukabiliana na Maafa katika Ukumbi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Maisara, mjini Unguja.

Mkurugenzi huyo pia aliwataka wafanyakazi hao kuwa mabalozi wazuri kwa kuyafikisha mafunzo hayo mpaka katika ngazi za familia ili jamii iwe na uelewa mpana katika kukabiliana na majanga.

Alisema yapo majanga ambayo husababishwa na binadamu wenyewe, hivyo ni vyema kuchukuliwe tahadhari za makusudi ili kupunguza athari katika jamii.

Wakitoa mada ya kukabiliana na maafa, watendaji kutoka Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa, Aziza Ali Rajab na Suleiman Kheir, waliwataka wafanyakazi hao kufuata taratibu na kuepuka majanga ambayo husababisha kutokea kwa maafa yakiwamo ya moto na maradhi ya mlipuko.

Pia walitaka taasisi za serikali na taasisi binafsi kuandaa mpango maalum wa kujiokoa wakati wa majanga na maafa ili kurahisisha uokozi pindi majanga yanapotokea.

Akitoa elimu ya kukabiliana na majanga ya moto, Ofisa Mkaguzi kutoka Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, Idrisa Khamis Mwinyi, aliitaka jamii kutoa ushirikiano katika kukabiliana na majanga yanapotokea.

Alisema watendaji wa kikosi hicho wamekuwa wanakabiliwa na changamoto ya kupitisha magari yao katika kuwahi sehemu yalikotokea majanga ya moto kutokana na wananchi kuweka vizuizi, hivyo magari yao kushindwa kupita na kufanya kazi zao.

# Ahukumiwa kifungo cha miaka 30 gerezani kisa bangi kilo 15

**Na Said Hamdani, LINDI**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Lindi imemuhukumu mkazi wa Kijiji cha Namkongo, Tarafa ya Nangaru, Salum Dadi (41) kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani baada ya kupatikana na hatia ya kumiliki kilo 14.8 za dawa ya kulevya aina ya bangi.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Maria Batraine baada ya kuridhishwa pasipo na shaka ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka uliokuwa umewasilishwa mbele ya mahakama hiyo.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea, akiiomba mahakama isimpe adhabu kali kwa kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza, ana familia wakiwamo watoto wawili, mke na wazazi wanaomtegemea.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Batraine alimwuliza Mwanasheria wa Serikali, Johan Odhiambo kama ana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshtakiwa, naye akidai hana, lakini akaiomba mahakama itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya kutumia dawa za kulevya kuharibu akili za wenzao.

Odhiambo alidai matumizi ya bangi huharibu akili za vijana ambao ni nguvukazi ya taifa na kuwafanya wawe tegemezi kwa jamii.

Hakimu Batraine, akitoa hukumu ya kesi hiyo namba 39/2023, alirejea Kifungu cha 15A (1)na (2)(c) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019, akisema amesikiliza maombi ya pande zote mbili, lakini sheria inamfunga mikono. Akamhukumu kifungo cha miaka 30 gerezani.

Awali ilidaiwa mahakamani huko na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Johan Odhiambo, kwamba mshtakiwa alikamatwa Agosti 10, 2023 nyumbani kwake Kijiji cha Namkongo, Tarafa ya Nangaru na askari polisi waliokuwa katika majukumu yao ya kazi akiwa anamiliki kilo 14.8 za dawa za kulevya aina ya bangi.

Alidai kwamba mshtakiwa aliweka bangi hiyo kwenye ndoo nane za plastiki zenye ujazo wa lita 10 na nyingine kwenye kiroba.



Mwenyekiti wa Umoja wa Benki Tanzania (TBA), Theobald Sabi (katikati), akibadilishana mawazo na baadhi ya wanachama na wageni waalikwa muda mfupi kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Pili wa Ujumuishi wa Kifedha uliofanyika jiijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Mkutano huo umeandaliwa na TBA na ulifunguliwa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bilioni 1.8/- kukarabati barabara zilizoharibiwa

**Na Beatrice Moses**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam imetenga Sh. 1.8 bilioni kwa ajili ya ukarabati wa barabara za mitaa yake zilizoharibika na mvua.

Barabara hizo ni zile ambazo haziko chini ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) au Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD).

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashim Komba, akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, alisema mchanganuo wa mgawanyo wa fedha hizo zitakavyotumika katika ukarabati wa barabara hizo utatolewa baadaye. Sasa wako kwenye hatua za awali za kubaini hali ya uhitaji wa gharama za matengenezo kwa barabara zilizoharibika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa awali na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa vyombo vya habari, halmashauri imetenga fedha hizo ambazo zitapelekwa kwenye kata na baadaye makandarasi kuanza kufanya kazi. Wanaamini barabara nyingi zitaanza kupitika, hivyo huduma ya usafiri kuwa ya uhakika.

"Tunaomba wananchi kuendelea kuwa na uvumilivu wakati jitihada hizi za serikali zikiendelea kufanyiwa kazi ili kutatua changamoto za ubovu wa miundombinu ya barabara," ilibainishwa



Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashim Komba

# DAS awaonya watumishi kushiriki Nanenane bila bidhaa ya kuonesha

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

KATIBU Tawala Wilaya ya Kibaha, Moses Magogwa, amewataka watumishi wa halmashauri ya wilaya hiyo kuzingatia ushiriki wao katika maonesho ya Nanenane kwa kuonesha mazao yanayolimwa katika maeneo yao.

Magogwa amesema ni vyema wakaondokana na tabia ya kwenda kwenye maonesho na kutembelea mabanda ya wengine badala yake wawe na kitu cha kuonesha kwenye maonesho hayo.

Alielekeza hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza kwenye Baraza Maalum la Madiwani lililoketi kupitisha makisio ya mpango wa bajeti wa mwaka 2024/25.

"Kilimo kinacholimwa katika Halmashauri ya Wilaya yetu kionekane kwenye maonesho, vitu vipandwe kipindi hiki tujiandae mapema tusiwe wa kwenda kutembelea mabanda ya wengine," aliagiza.

Pia alielekeza kuwekwa utaratibu wa kutenga muda wa kufanya mikutano ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi wa haraka.

Baraza hilo lilipitisha makisio ya Sh. bilioni 34.9 kwa ajili ya mpango wa bajeti wa mwaka 2024/25, zikielekezwa kutumika wenye utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Kati yake, Sh. bilioni 2.5 ni makusanyo ya ndani, vyanzo visivyo na masharti Sh. bilioni 1.5, makusanyo yatokanayo na Mfuko wa Afya wa Jamii, ada, bima, malipo ya papo kwa papo, ada ya taka ngumu na duka la dawa, Sh. 19.73 ni mishahara ya watumishi, Sh. bilioni1.5 ni matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 10.3 ni miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Erasto Makala, alisema kati ya fedha hizo zaidi ya Sh. bilioni moja ni kupitia fedha za mapato ya ndani, Sh. bilioni 5.9 ni fedha za miradi za ndani (Serikali Kuu) na Sh. bilioni 3.3 ni fedha za wahisani.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Edward Masona alisema watahakikisha wanaimarisha ukusanyaji mapato ya ndani kwa kutenga fedha na kupeleka kwenye miradi ya maendeleo.

# Gekul aitwa Mahakama Kuu kujibu rufani yake

**Na Mwandishi Wetu,**
BABATI

MBUNGE wa Babati Mjini (CCM), Pauline Gekul ameitwa Mahakama Kuu Kanda ya Babati, mkoani Manyara kujibu rufani iliyofunguliwa dhidi yake na Hashim Ally kupitia Wakili wake, Peter Madeleka.

Gekul ameitwa kwa hati ya wito mahakamani huko Machi 18, mwaka huu kwa ajili ya kusikiliza rufani hiyo namba 577 ya mwaka 2024 chini ya Jaji Stephen Magoiga.

Katika shauri la msingi, mbunge huyo alifutiwa kesi ya unyanyasaji dhidi ya mfanyakazi wake Hashim Ally na Mahakama ya Wilaya ya Babati baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DDP) kuwasilisha taarifa ya kutokuwa na nia ya kuendelea na shauri hilo.

DPP aliwasilisha taarifa hiyo ya kutokuwa na nia ya kuendelea na kesi hiyo chini ya kifungu cha 91 (1) cha CPA kinachompa mamlaka ya kufuta kesi yoyote ya jinai katika hatua yoyote kabla ya hukumu ya mahakama na bila kulazimika kutoa sababu za uamuzi huo.

Kesi ya msingi ilifunguliwa na Hashim kupitia kwa Wakili Madeleka chini ya Kifungu cha 128(2) na (4) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2022.

Wakati kesi hiyo inafunguliwa Mahakama ya Wilaya ya Babati, Wakili Madeleka, alidai kifungu hicho kinaruhusu mtu binafsi kufungua kesi ya jinai bila kupitia kwa DPP.

Katika shauri la msingi, Gekul alikuwa anakabiliwa na shtaka moja la shambulio na kusababisha madhara kwa mwili chini ya Kifungu cha 241 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2022.

Ilidaiwa kuwa yeye na watu wengine ambao hawako katika malalamiko hayo, Novemba 11, 2023, mjini Babati, walimwita Hashim na kumweka kizuizini.

Ilidaiwa kuwa huku wakimtishia kwa silaha ya moto, walimvua nguo na kumshambulia kwa kumlazimisha kukalia chupa ya soda ili iingie katika njia yake ya haja kubwa.



Hali ilivyo nchini Senegal baada ya vyama vya upinzani kuitisha maandamano kupinga kuahirishwa kwa uchaguzi mkuu. **PICHA: MTANDAO**

# Israel yazidi kunyooshewa kidole vita Gaza

**GAZA,** PALESTINA

ISRAEL imezidi kukabiliwa na ongezeko la onyo la kimataifa kuhusu mpango wake wa kushambulia Rafah, mji ulioko kusini mwa Ukanda wa Gaza uliojaa wakimbizi wa Kipalestina.

Onyo hiyo imetolewa baada ya Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, kuamuru jeshi lake kujiandaa kuwahamisha raia kutoka mji huo kabla ya mashambulizi makubwa dhidi ya Hamas, baada ya kukataa mapendekezo ya kundi hilo juu ya kusitisha mapigano.

"Haiwezekani kufikia lengo la vita bila ya kuwaondoa Hamas na kwa kuacha vikosi vinne vya Hamas huko Rafah. Ni wazi kwamba shughuli kali huko Rafah wananchi wanahitajika kuondoka katika maeneo ya mapigano," ilisema ofisi ya Netanyahu.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, David Cameron, alisema zaidi ya nusu ya wakazi wa Gaza wanajihifadhi katika eneo hilo, huku Saudi Arabia ikionya kuhusu athari mbaya zitakazojitokeza endapo Rafah itavamiwa.

Marekani tayari imeonya Israel kwamba uvamizi wa Rafah kama sehemu ya shambulio lake dhidi ya Gaza utakuwa janga, wakati Umoja wa Ulaya (EU) na Umoja wa Mataifa (UN) zote zikionesha wasiwasi wao.

Mashirika ya misaada pia yalisema kuwa haiwezekani kuwahamisha kila mtu kutoka katika mji huo ulio kwenye mpaka na Misri. Na kwamba takribani Wapalestina milioni 1.5 wanaaminika kuwa mjini Rafah, wakitafuta hifadhi kutokana na operesheni za kivita za Israel katika maeneo mengine ya Ukanda wa Gaza, huku wengi wao wanaishi kwenye mahema.

Watawala wa Ukanda wa Gaza kundi la Hamas walisema kunaweza kuwapo maelfu ya majeruhi endapo eneo hilo litashambuliwa.

Israel ilianzisha operesheni zake katika eneo la Palestina baada ya zaidi ya watu 1,200 kuuawa kusini mwa Israel Oktoba 2023 na watu wenye silaha wa Hamas.

Aidha, ilielezwa kuwa zaidi ya watu 27,900 wameuawa na takribani 67,000 kujeruhiwa huko Gaza tangu wakati huo, kulingana na Wizara ya Afya inayoendeshwa na Hamas.

**VIFO VYAONGEZEKA**

Hata hivyo Wizara ya Afya huko Gaza inayodhibitiwa na Hamas ilisema zaidi ya watu 28,000 wameuawa katika eneo hilo lililozingirwa tangu kuanza kwa vita kati ya Israel na kundi hilo la wanamgambo.

Ilielezwa kuwa idadi ya hivi karibuni ya waliouawa imetokana na vifo vya watu 117 ndani ya kipindi cha saa 24 zilizopita. Huku taarifa ya wizara hiyo ikisema watu wengine 67,611 wamejeruhiwa mjini Gaza tangu kuanza kwa vita hivyo Oktoba 2023.

Vile vile, wakati mapigano yakiendelea, Jeshi la Israel lilisema linachukua hatua kuepuka mauaji ya wananchi katika operesheni yao wanayosema inawalenga wanamgambo wa Hamas. **BBC, DW**

# Uwekezaji mdogo sekta binafsi wamshtua waziri

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amesema kiwango cha uwekezaji kinachofanywa na sekta binafsi ni kidogo kwenye sekta mbalimbali nchini.

Prof. Mkumbo alitoa kauli hiyo jana Dar es Salaam wakati akifungua warsha ya kimkakati ya wadau wa maendeleo wa sekta ya usafirishaji.

Alisema katika kipindi cha kuandika Dira mpya ya Maendeleo ya Taifa na kuelekea Bunge la Bajeti ni vyema wadau hao wakatoa mapendekezo ya namna ambavyo wanataka dira hiyo iseme.

"Uwekezaji wote ambao umefanywa mpaka sasa ni wa sekta ya umma, mchango wa sekta binafsi katika eneo hili bado ni mdogo, hivyo tunataka wajadiliane hasa ni kwa namna gani sekta hiyo itashiriki kuwekeza katika maeneo mbalimbali ikiwamo kuboresha miundombinu yetu ya usafiri hususani barabara, maji na maeneo mengineyo.

"Matarajio yetu kama serikali ni kwamba mwisho wa kikao hiki watatuletea taarifa na mapendekezo mazuri hasa katika kipindi hiki ambacho tunaelekea katika Bunge la Bajeti, ili yaingie kwenye mpango wa maendeleo kwa sababu tupo katika mpango wa kuandika Dira mpya ya Maendeleo," alisema.

Mkurugenzi wa Kituo cha Ubia, David Kafulila, alisema mpaka sasa sehemu kubwa ya ujenzi wa uchumi inafanywa na serikali yenyewe. Lengo ni kuhakikisha sekta binafsi nayo inatoa mchango wake kupitia uwekezaji kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Tunataka sehemu kubwa ya uchumi ijengwe na sekta binafsi kwa sababu mpaka sasa sehemu kubwa ya ujenzi wa uchumi huo inafanywa na serikali yenyewe. Sisi tunataka sekta binafsi nayo itoe mchango wake.

"Mimi kama mkurugenzi wa kituo cha ubia, kazi yangu ni kuunganisha fursa ambazo ziko serikalini kwenye sekta binafsi ili wazichukue na kuzitumia. Kwenye ubia ni kwamba sekta binafsi zinafanya kazi ambazo serikali inapaswa kufanya, mfano kujenga barabara."

"Tunayo kazi ya kufanya kuhakikisha kuwa ukuaji uchumi unajengwa na sekta binafsi, tunapaswa kuhakikisha katika miaka mitano, mitaji kutoka sekta binafsi inayotekeleza miradi ya serikali kwa utaratibu wa ubia inafikia thamani ya Sh. trilioni 21. Alisema vipaumbele vyao ni katika sekta ambazo zinachukua fedha nyingi za serikali ikiwamo sekta ya ujenzi na nishati.

Alisema kitendo cha Rais Samia Suluhu Hassan kuruhusu kufanyika mabadiliko ya sheria ya ubia, kutasaidia kuleta ushindani na kuvutia wawekezaji nchini na pia kuipunguzia serikali mzigo wa kufanya kila kitu.

"Lengo ni kuhakikisha serikali inaachana na kufanya kazi ambazo zinaweza kufanywa na sekta binafsi. Wawekezaji wa ndani na nje wanahitaji mazingira rafiki ya uwekezaji," alisema Kafulila.

# TWIGA STARS KAMBINI KUIWINDA BANYANA BANYANA OLIMPIKI

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha wachezaji 24 wa Timu ya Taifa ya Wanawake 'Twiga Stars', kinachonolewa na Kocha Bakari Shime, kimeingia kambini jijini Dar es Salaam jana tayari kwa ajili ya kujiandaa kwa mchezo wa kufuzu Olimpiki dhidi ya Afrika Kusini, 'Banyana Banyana'.

Twiga Stars itakuwa ugenini dhidi ya wenyeji hao, Banyana Banyana, Februari 19 na 28, mwaka huu watarudiana katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, katika kinyang'anyiro hicho ambacho kina jumla raundi ya nne za mchujo na mwishowe timu mbili zitaiwakilisha Afrika kwenye michuano hiyo itakayofanyika mwakani jijini Paris, Ufaransa.

Twiga Stars imefanikiwa kutinga raundi ya tatu ya mchujo wa kuwania tiketi ya michuano hiyo ya Olimpiki baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wenyeji, Botswana katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Taifa jijini Gaborone nchini humo, bao hilo pekee likifungwa na mshambuliaji anayeichezea BK Hacken ya Sweden, Aisha Masaka.

Akizungumza na Nipashe jana, Shime, alisema amefanikiwa kupata nyota wake ambao wanacheza soka la kulipwa baada ya baadhi ya nchini ligi zao kusimama na nyota hao kuweza kujiunga mapema na timu zao za taifa.

Alisema wamechelewa kuingia kambini kulingana na ligi ya mataifa mengi ilikuwa ikiendelea lakini kwa sasa zimesimama na baadhi ya wachezaji kujiunga na timu zao.

"Hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu ya ubora wa wachezaji wao, lakini ninaimani na vijana wangu tunaweza kufanya vizuri, kwa sasa ni kuhakikisha tunajiandaa vizuri na kuweka mpango mkakati kuelekea mechi yetu dhidi ya Afrika Kusini," alisema kocha huyo.

Kikosi cha Twiga Stars kinaundwa na makipa; Najat Abasi (JKT Queens), Asha Mrisho (Aman Queens) na Husan Mtunda (Yanga). Mabeki ni Julietha Singano (Juarez, Mexico), Anastazia Katunzi, Christer Bahera, Happy Hezron (JKT Queens), Fatuma Issa na Violeth Nicholaus (Simba Queens).

Viungo ni Ester Mabanza, Stumai Abdallah, Joyce Lema, Jamet Christopher na Amani Bilal (JKT Queens), Aquila Gaspar (Fountain Gate Princess), Hasnat Ubamba na Irene Kisisa (Yanga), Enekia Kasonga (Eastern Flames- Saudia Arabia) na Diana Lucas (Ame S.F.K- Uturuki).

Safu ya ushambuliaji inaundwa na Opa Clement (Besiktas - Uturuki), Aisha Juma (Simba Queens), Donisia Minja, Winifrida Gerald na Jamila Rajabu (JKT Queens ).

**TUPO TAYARI...**




Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini jana kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Geita Gold FC, itakayopigwa Uwanja wa CCM Kirumba leo. **PICHA: SIMBA**

# JKU yajivunia soka safi ikivutwa shati Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya vinara wa Ligi Kuu Zanzibar, JKU SC kupunguzwa kasi ya mbio za kuusaka ubingwa wa ligi hiyo kwa kukubali kupokea kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Wanajeshi wa Mipakani, Uhamiaji FC, wamesema soka walilicheza, lakini bahati haikuwa upande wao.

Bao pekee lililoharibu mipango ya Maafande wa JKU SC, lilipachikwa nyavuni na Ali Khatibu katika dakika ya 35.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu ya JKU SC, Salum Haji, alisema haikuwa bahati yao kupata ushindi katika mchezo huo licha ya wachezaji kuonesha kiwango safi.

Alisema karibu dakika zote timu yake ilimiliki mchezo huo katika nafasi zote, lakini haikuwa bahati yao kupata alama tatu.

Alisema hawezi kusema kuwa goli lililofungwa limesababishwa na safu yake ya ulinzi au mabeki bali ni makosa tu madogo mchezo wa kawaida ambayo yalitokea na kusababisha kuadhibiwa na wapinzani wao.

Alisema kupoteza mchezo huo kumezidi kumpa nguvu ya kuhakikisha wachezaji wake wanafanya vizuri katika mechi yao ujao ili kuendeleza mipango yao ya mbio za ubingwa.

"Mechi ilikuwa ngumu sana na kama mnavyojua tupo katika mzunguko wa lala salama za ubingwa na kusalia Ligi Kuu, hivyo michezo yote tunayocheza kila timu inaangalia nafasi yake ili kuhakikisha inajiimarisha sehemu ilipo,"alisema.

Aidha, alisema wamecheza na timu ambayo inahitaji kupata matokeo ili kujinusuru kuingia katika mstari wa kushuka daraja, hivyo alitarajia mchezo huo kutokea mabadiliko yoyote ya kimbinu uwanjani.

"Wapinzani wetu hawapo katika nafasi nzuri sana baada ya mzunguko wa kwanza kuambulia sare nyingi, lakini pia mzunguko wa pili mchezo wa kwanza haikufanya vizuri, hivyo nilitarajia kwa mchezo huu lolote litatokea," alisema.

Vinara hao wa Ligi Kuu ya Zanzibar wana alama 39, katika michezo 17 waliyocheza ambapo wamefungwa michezo miwili , wametoka sare tatu na wameshinda michezo 12, wakati wapinzani wao Uhamiaji FC wakifikisha alama 22 wakiwa nafasi ya saba wameshinda minne, wametoka sare 10 na wamefungwa mechi tatu.

## Waandishi michezo kunolewa kwa Afcon

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Tanzania ikiwa inajiandaa na uwenyeji wa Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027, serikali kuandaa mafunzo maalum kwa waandishi wa habari za michezo nchini, yatakayowasaidia kuripoti kwa weledi mashindano hayo ambayo yatafanyika kwa ushirikiano wa nchi tatu zikiwamo Kenya na Uganda.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ambaye alimwakilisha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, katika Bonanza la Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo (Taswa), lililofanyika kwenye viwanja vya Fukwe za Msasani, Dar es Salaam.

„Serikali itahakikisha waandishi wa habari za michezo hapa nchini mnapata mafunzo nje na ndani ya nchi ikiwamo vitendea kazi ambavyo vitawafanya mpate uzoefu wa kuripoti vizuri mashindano hayo," alisema Nnauye.

Aidha, Waziri Nape aliipongeza TASWA kwa kuandaa bonanza hilo ambalo halijafanyika kwa kipindi kirefu, ikiwa ni pamoja na kurudisha tunzo ya mchezaji bora kila mwezi.

Alisema ataandaa tunzo kubwa zenye ubora ambazo hazijawahi kutolewa ili kuwapa moyo wachezaji kuzidi kufanya vema kwenye mashindano mbalimbali kupitia chama hicho.

## Chipukizi matumaini kibao Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa Chipukizi FC, Abdallah Mzee, amesema anakiamini kikosi chake kinaweza kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu Zanzibar katika mzunguko huu wa lala salama licha ya juzi kukubali kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Maafande wa KVZ katika mchezo wa 16 wa ligi hiyo uliochezwa katika Uwanja wa Mau B visiwani hapa.

Akizungumzia mchezo huo, Mzee alisema walifungwa katika dakika ya mwishoni kutokana na makosa madogo yaliyofanywa na walinzi wake.

Alisema kupoteza umakini kwa safu ya ulinzi ndiko kulikosababisha dhahama hiyo dakika za mwisho baada ya kutoshana mabavu tangu mwanzo wa mchezo huo.

Alisema siku zote unapocheza na timu ambayo ipo katika mbio za ubingwa mchezo huwa mgumu na hutumika kila mbinu za kiuchezaji ili kupata matokeo mazuri.

"Wachezaji wangu walicheza vizuri katika dakika zote za mchezo, hata goli tulilofungwa lilikuwa la bahati mbaya sana, walinzi walijisahau wakazidiwa mbinu tukafungwa," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE MKATABA MPYA

KLABU ya Paris St-Germain imempa mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, mkataba mpya wa miaka miwili wenye thamani ya pauni milioni 136 kwa matumaini ya kumshawishi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, kukataa kuhamia Real Madrid. **(AS)**

### ARSENAL YATUMA MASKAUTI

KLABU ya Arsenal ilituma maskauti kwa Molineux Jumamosi kuwatazama winga wa Wolves na Ureno, Pedro Neto na mshambuliaji wa Brentford, Ivan, 27. **(HITC)**

### BARCA NA ONANA

VIZUIZI vya kifedha vya Barcelona vinamaanisha kuwa wataingia tu kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua Amadou Onana wa Everton ikiwa ,The Toffees' hao watapunguza dau la pauni milioni 51 kumnunua kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 22, ambaye anazivutia Manchester United, Arsenal na Chelsea. **(Sun Sunday)**

### GUDMUNDSSON AWINDWA

KLABU ya Newcastle United na Tottenham Hotspur zinafikiria kumnunua mshambuliaji wa Genoa na Iceland, Albert Gudmundsson, mwenye umri wa miaka 25, msimu wa majira ya joto. **(Calciomercato)**

### OSMAN SASA KUUZWA

KLABU ya Brighton iko tayari kumuuza Kaoru Mitoma msimu huu wa majira joto kufuatia kumsajili winga wa Ghana, Ibrahim Osman, mwenye umri wa miaka 19, huku Barcelona, Manchester City, Manchester United na Chelsea wakihusishwa na mshambuliaji huyo wa Japan mwenye umri wa miaka 26. **(Football Transfers)**

### KIWIOR ATAKIWA SEVILLA

SEVILLE inataka kumsajili mlinzi wa Arsenal, Jakub Kiwior mwenye umri wa miaka 23, ambaye anavutiwa na AC Milan. **(Fichajes)**

### HERRMANN AFUATILIWA

BRIGHTON ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England zinazomfuatilia mlinzi wa Borussia Dortmund, Charles Herrmann,18. **(Florian Plettenberg)**

### MASTERS ASHINIKIZWA

MTENDAJI Mkuu wa Ligi Kuu England, Richard Masters, yuko chini ya shinikizo kutoka kwa kundi la klabu zisizofurahishwa na uongozi wake kuhusu masuala kadhaa. **(Mail Sunday)**

### GALLAGHER KUUZWA

CHELSEA itajaribu kusawazisha vitabu vyao msimu utakapomalizika kwa kumuuza kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 24 na nyota wengine wengi. **(Football Insider)**

### JONG AFUATILIWA

CHELSEA, Manchester United na Paris St-Germain zinamfuatilia kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 26, huku kukiwa na sitofahamu kuhusu mustakabali wake pale Barcelona. **(Sport)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CHELSEA SASA YAPANIA KUMTOA DE JONG BARCA

Euro milioni 100 kutumika kuinasa saini yake wakati huu ambao naye...

**LONDON, England**

FRENKIE de Jong anazidi kukatishwa tamaa na maisha ya Barcelona na Chelsea inaweza kumpa njia ya kuondoka kwa dau la uhamisho wa euro milioni 100 msimu wa majira ya joto, kwa mujibu wa ESPN.

Muda wa Mholanzi huyo akiwa pale Katalunya unakabiliwa na nia ya kutaka huduma yake kutoka kwa timu kama Manchester United, ingawa sasa yuko katika msimu wake wa tano na Barca tangu asajiliwe kutoka Ajax mwaka 2019 kwa euro milioni 75.

De Jong siku zote amekuwa akitaka kubaki na wababe hao wa LaLiga licha ya nia ya Barca kumuuza katika miaka ya hivi karibuni, lakini ESPN inasema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, anaweza kuondoka msimu wa majira ya joto.

Kiungo huyo anasemekana kusikitishwa na kiwango cha ,Blaugrana' hao kwenye LaLiga, huku wakipokea kichapo kwenye Supercopa de Espana na Copa del Rey.

Kocha Xavi tayari amethibitisha kuwa atajiuzulu nafasi yake mwishoni mwa msimu huu.


ESPN imeongeza kuwa Mkurugenzi wa Michezo, Deco amejaribu kujadili tena kuongeza mkataba wa De Jong hadi mwaka 2029, lakini hadi sasa imekuwa ,haiwezekani' kufikia makubaliano.

Inadaiwa kuwa Chelsea ya Mauricio Pochettino itakuwa tayari kutumia euro milioni 100 kumsajili De Jong, ikiwa tayari Enzo Fernandez, Moises Caicedo na Romeo Lavia wamegharimu kiasi kikubwa cha fedha.

,The Blues' walifanya vibaya katika dirisha la usajili la Januari na wanasemekana kuhofia kukatwa pointi iwapo watamtimua Pochettino na wafanyakazi wake, ikizingatiwa kuwa wanaweza kukiuka kanuni za Faida na Uendelevu (PSR).

Man Utd bado walikuwa na nia ya kumnunua De Jong msimu uliopita wa majira ya joto, huku Bayern Munich nao walikuwa pia pamoja na Paris Saint-Germain.

KOCHA wa Afrika Kusini, Hugo Broos, amewasifu wachezaji wake baada ya mechi yao kali kumalizika kwenye...



## Trent Alexander-Arnold aweka rekodi asisti EPL

**LIVERPOOL, England**

TRENT Alexander-Arnold aliweka rekodi ya kuwa beki aliyetoa pasi nyingi za mabao kwenye Ligi Kuu England katika ushindi wa 3-1 wa Liverpool dhidi ya Burnley, juzi.

Pasi ya Alexander-Arnold iliwekwa wavuni na Diogo Jota na kufungua ukurasa wa mabao na kufungua vitabu vya historia kwa beki huyo wa kulia wa Liverpool, ambaye sasa ametengeneza mabao 58 katika maisha yake yote ya Ligi Kuu England.

Ameipiku rekodi kutoka kwa mchezaji mwenzake, Andy Robertson, ambaye ana asisti 57. Robertson alivunja rekodi ya awali alipoipita ile ya Leighton Baines aliyetoa pasi 53 za mabao Desemba, 2022 lakini kutokana na kukaa nje kwa muda kutokana na jeraha la bega kumemruhusu Alexander-Arnold kushika rekodi hiyo.

Asisti hiyo ilikuwa ya nne kwa Alexander-Arnold msimu huu na ya kumi katika mashindano yote.

Kwa upande mwingine wa wigo, Robertson bado anasubiri pasi yake ya kwanza ya goli kwenye kampeni, akiwa amecheza mechi 11 pekee kwenye ligi msimu huu.

Hatua iliyo mbele ya Robertson pia inamfanya Alexander-Arnold kuwa muundaji wa tatu katika historia ya Ligi Kuu ya Liverpool.

Steven Gerrard anaongoza chati akiwa na asisti 92, huku Mohamed Salah akimfuata kwa kuwa na 66.

Alexander-Arnold pia anashikilia rekodi ya kutoa pasi nyingi zaidi kama beki katika msimu mmoja wa Ligi Kuu, akiiweka mwaka 2019 kabla ya kuivunja mwenyewe kwani alitengeneza nafasi 13 mnamo Julai 2020.

Baada ya kupachika mabao mengine 12 msimu wa 2021/22, Alexander-Arnold alivumilia kushuka kwa kiwango chake msimu uliopita, lakini aliendelea kufurika hadi mwisho wa kampeni, akitoa pasi saba za mabao katika mechi kumi za mwisho na kumaliza na mabao tisa.

# KOCHA AKOSHWA AFRIKA KUSINI 3-BORA

**ABIDJAN, Ivory Coast**

KOCHA wa Afrika Kusini, Hugo Broos, amewasifu wachezaji wake baada ya mechi yao kali kumalizika kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), dhidi ya DR Congo na kufanikiwa kutwaa nafasi ya tatu.

Kwenye mchezo huo timu hizo hakizufungana katika muda wa kawaida wa dakika 90 na mshindi akaamuliwa kwa changamoto ya mikwaju ya penalti na Afrika Kusini ikashinda penalti 6-5.

Huku kikosi chake kikiwa na nafasi chache sana, Broos alifurahishwa na ushindi huo kwa kuwasambaratisha Congo ambao ni moja ya vigogo wa soka Afrika.

Akizungumza baada ya kushika nafasi ya tatu mjini Abidjan, Broos alikimwagia sifa kemkem kikosi chake kwa waliopambana uwanjani na wale waliokuwa benchi.

"Nilisema baada ya mechi ya Nigeria kwamba ninajivunia timu hii, na nadhani leo (juzi) watu wanaweza kuona kwa nini nasema ninajivunia timu hii. Hatukuwa wapya, lakini unapoona mawazo katika kundi hilo, ni ya kuvutia," alisema kocha huyo.

"Vijana walifanya vizuri sana. Walionesha akili kubwa. Walijaribu kufanya kile nilichowaambia, na ninaelewa kuwa ilikuwa ngumu. Inaonesha kwamba sisi tukiwa na matatizo, tunaweza kuwategemea wale walio kwenye benchi.

"Niliridhika na wachezaji uwanjani, lakini niliridhika zaidi na wale waliokuwa benchi. Walikuwa wakiwatia moyo na kuwasukuma. Kutokana na hili, unajua kwamba una vijana 23 ambao wanataka kitu kimoja na ambacho ni kushinda," aliongeza kocha huyo.

Mashindano ya Afcon yalikamilika jana Jumapili baada ya mechi ya fainali kati ya Nigeria na wenyeji, Ivoty Coast.

# BELLINGHAM AZUA HOFU MADRID

**MADRID, Hispania**

JERAHA la kifundo cha mguu la Jude Bellingham lilipunguza furaha ya Real Madrid wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Girona kwenye Uwanja wa Bernabeu, juzi.

Kikosi cha Carlo Ancelotti kilitunisha msuli kwenye ardhi ya nyumbani na kusonga mbele kwa pointi tano kileleni mwa msimamo wa LaLiga - na pointi 11 mbele ya wapinzani wao Barcelona.

Vinicius Junior alifunga bao la kwanza baada ya dakika sita pekee kwa shuti kali la mguu wa kulia kabla ya Bellingham, katika onyesho lingine la kuvutia la mtu binafsi, kufikisha mabao 16 kwenye ligi.

Hata hivyo, nyota huyo wa England mwenye umri wa miaka 20, alilazimika kuondoka uwanjani kabla ya bao la Rodrygo Goes dakika ya 61 baada ya kuumia kwenye kifundo cha mguu wake wa kushoto wakati akikabana na mshambuliaji wa Girona, Pablo Torre.

Bellingham alitibiwa na aliweza kuendelea kucheza kwa muda mfupi, hata akafunga bao lake la pili la mchezo kabla ya kukaa kwenye uwanja na kuomba nafasi ya kutoka nje na nafasi yake kuchukuliwa na Brahim Diaz.



Bosi wa Real Madrid, Ancelotti alithibitisha kwamba nyota huyo wa zamani wa Birmingham aliumia kifundo cha mguu na kwamba atapimwa zaidi.

Iwapo uchunguzi utathibitisha jeraha hilo ni kubwa kuliko ilivyofikiriwa, litakuwa pigo kubwa kwa Real Madrid kabla ya kipindi muhimu katika msimu wao.

'Los Blancos' watasafiri hadi RB Leipzig Jumanne kwa mchezo wa mkondo wa kwanza wa hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya safari ya LaLiga dhidi ya Rayo Vallecano wikendi.

Bellingham amekosa mechi tano pekee katika mashindano yote msimu huu baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 88.5 kutoka Borussia Dortmund majira ya joto yaliyopita.

# RUVU SHOOTING YASHINDA BAADA YA MICHEZO 20

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE timu ya Ruvu Shooting, juzi ilipata ushindi wake wa kwanza kwenye Ligi ya Championship, ilipoifunga Mbuni FC mabao 2-1 katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Ni ushindi wa kwanza kwa timu hiyo baada ya kucheza michezo 20 bila kuondoka na pointi tatu.

Ruvu Shooting iliyoshuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu uliopita, ndiyo timu pekee iliyocheza mzunguko wote wa kwanza wa ligi bila kupata ushindi.

Awali, ilikuwa imecheza mechi 20, ikipoteza michezo 16 na sare nne, kabla ya juzi kucheza mechi ya 21 ambayo imezoa pointi zote tatu.

Hata hivyo, matokeo hayo hayajaiwezesha timu hiyo hata kujitikisa kwenye nafasi ya mwisho ya msimamo wa ligi hiyo, ikiwa ina pointi saba tu katika michezo iliyocheza mpaka sasa.

Wakati Ruvu Shooting ikikumbuka shuka kumekucha, timu ya Pamba FC ilipunguzwa kasi na kulazimishwa suluhu dhidi ya Green Warriors, mechi ikipigwa Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Matokeo hayo yanaifanya timu hiyo kufikisha pointi 44 ikiwa kwenye nafasi ya pili ya msimamo, ikitoa mwanya kwa Biashara United kama itashinda mechi yake dhidi ya FGA Talents kukwea hadi nafasi ya pili kwani itakuwa imefikisha pointi 46.

Timu nyingine iliyoshuka daraja msimu uliopita kutoka Ligi Kuu, Polisi Tanzania ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Stand United. ikiwa ugenini, Uwanja wa Mwadui Complex, Shinyanga.

Mpaka kufikia raundi ya 21, Polisi Tanzania ipo nafasi ya nane na pointi zake 29, Stand United ikiwa nafasi ya tisa, ikikusanya pointi 25.

**KAZI KAZI...**




Mshambuliaji mpya wa Yanga, Joseph Guede, akimiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Tanzania Prisons kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya jana na Yanga kushinga mabao 2-1. **MPIGAPICHA WETU**

# Washindi 'Twende Afcon na Betway washuhudia fainali

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Dodoma, Prisca Sospeter, ameishuhudia mechi ya fainali mashindano ya Kombe la Mataifa ya Africa (AFCON) jana, kati ya Nigeria na wenyeji, Ivory Coast iliyopigwa nchini humo.

Prisca alipata fursa ya kushuhudia mechi hiyo ya fainali kupitia Promosheni ya 'Twende AFCON na Betway', hiyo ikiwa ni awamu ya pili kwa kampuni hiyo ya kubashiri kupeleka washindi kushuhudia michuano hiyo.

Promosheni hiyo iliyozinduliwa Novemba mwaka jana, pamoja na mambo mengine ilikuwa na lengo la kuwapatia fursa Watanzania hususan watumiaji wa mtandao wa kubashiri wa Betway kwenda kuiunga mkono Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), iliyokuwa ikishiriki pia mashindano hayo.

Akizungumzia fursa hiyo kabla ya kuondoka kuelekea Ivory Coast juzi, Prisca alisema kwake imekuwa ni furaha kubwa kwenda kushuhudia michuano hiyo yenye thamani kubwa barani Afrika akiamini kuwa itamsaidia kumuongezea uelewa zaidi katika masuala ya soka la Afrika na ushindani uliopo baina ya nchi na nchi huku ikimpa nafasi ya kukutana na watu mbalimbali.

"Namshukuru Mungu kupata nafasi hii, kwangu ni mara ya kwanza kusafiri kwenda Ivory Coast, pia fursa ya kuiona michuano hii mikubwa mubashara nikiwa uwanjani wakati mchezo ukiendelea," alisema Prisca huku akiishukuru Betway Tanzania kwa kuleta Promosheni hiyo iliyompatia fursa hiyo.

Kwa upande wa Balozi wa Betway Tanzania, Salama Jabir, alisema promosheni hiyo iliyodumu kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia Novemba 16 hadi Desemba 16, ilikuwa na lengo la kuwapa fursa Watanzania kwenda nchini Ivory Coast kuishuhudia michuano hiyo, lakini pia kuipa sapoti Timu ya Taifa ya Tanzania ambayo tayari ilishayaaga mashindano hayo.

"Tunajua timu yetu ilikuwa Ivory Coast kushiriki michuano ya AFCON, kwa hiyo promosheni yetu iliienda na mkakati wa kuwawezesha Watanzania kwenda kuipa nguvu, lakini kwa bahati mbaya wapiganaji wetu waliondolewa, tunaamini wakati ujao itafanya vizuri zaidi na zaidi kwani hata mwaka huu imeonyesha nguvu kubwa,"alisema Salama.

Michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, ambayo jana usiku ilitamatika kwa kuchezwa mechi ya fainali kati ya Nigeria na wenyeji Ivory Coast, ilianza nchini humo Januari 13, mwaka huu ikijumuisha timu kutoka mataifa 24 ikiwamo Tanzania ambayo kwa hii ni mara ya tatu tangu ilishiriki kwa mara ya kwanza 1980 na 2019.

## Simba waahidi furaha kubwa

INATOKA UK. 24

Nahodha wa timu hiyo, Elius Maguli, alisema hawana sababu yoyote ya kutoshinda kwa sababu wanacheza wakiwa nyumbani.

Katika hatua nyingine, aliyekuwa mchezaji na Kocha wa zamani wa Simba, Abdallah Kibadeni, amewataka wachezaji wa timu hiyo, kujituma na kujitolea kwa ajili ya klabu, vinginevyo wataukosa ubingwa kwa mara nyingine tena msimu huu.

Kibadeni amesema wachezaji wa timu hiyo wanaonekana kama wamekuwa wakiridhika mapema hasa wanapokuwa wakipata ushindi katika mechi mbili mfululizo na kutoitolea macho mechi inayofuata.

Akizungumza na Nipashe jana, Kibadeni alisema wanatakiwa kujitoa na kupambana kwa ajili ya klabu kama ilivyo kwa Yanga, jambo ambalo anaamini wakifanya hivyo watafikia malengo yanayotarajiwa ikiwamo kutwaa taji la ubingwa wa ligi hiyo na kucheza nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema hana shida na uwezo wa benchi la ufundi la Simba linaloongozwa na Abdelhak Benchikha, ambaye amebadilisha timu yao kutoka kule kucheza kwa presha hadi sasa jambo ambalo linaangushwa na wachezaji kutojitoa na kupambana.

"Kuifunga Tabora United mabao 4-0 tuliona ni kipimo cha kuweza kupambana na timu kubwa, baada ya ushindi huo tukaona Azam FC ni sawa nao na kucheza kipindi cha kwanza kwa kuridhika na kuruhusu bao licha ya kusawazisha dakika za mwisho.

## Yanga SC kileleni raundi ya kwanza

INATOKA UK. 24

Prisons walionekana kuushika mchezo na kuwapa wakati mgumu wageni wao.

Kipa wa Yanga, Metacha Mnata alizawadiwa kadi nyekundu dakika ya 58 na mwamuzi Ahmed Aragija baada ya kumwangusha Mbangula aliyekuwa amemlamba chenga, madhambi ambayo yalitokea kwenye mstari unaotenganisha eneo la ndani ya penalti na nje.

Yanga ililazimika kumtoa Farid Mussa na kumwingiza Abutwalib Mshery ambaye kazi yake ya kwanza ilikuwa ni kuzuia faulo, ambayo awali mwamuzi alionyesha penalti kabla ya kubadilisha maamuzi.

Alikuwa ni Jeremiah Juma aliyepiga faulo hiyo kwa ustadi mkubwa, mpira ukajaa kushoto kwa kipa huyo akiwa amesimama tu.

Baada ya bao hilo, Prisons walicharuka kusaka la kusawazisha, lakini mabeki wa Yanga walikaa imara, hadi dakika nne kabla mechi kumalizika mchezaji wao Zabona Mayombya naye alipigwa kadi nyekundu kwa madai kujiangusha ndani ya eneo la hatari.

Michezo
Jumatatu Februari 12, 2024
Nipashe

Chelsea sasa yapania kumtoa De Jong Barca UKURASA 21



MNAHESABU?...



Pacome Zouzoua (katikati), akishangilia kwa staili yake sambamba na Farid Musa (kushoto) na Maxi Nzengeli, baada ya kuiandikia Yanga bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Tanzania Prisons katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya jana. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA SC KILELENI RAUNDI YA KWANZA

●●● Pacome aweka kamba ya nane Ligi Kuu huku Yao Kouassi akimfikia Kipre Junior wa Azam FC kwa...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wamemaliza mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo wakiwa kileleni mwa msimamo baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Prisons jana ulioiwezesha kuvuna jumla ya pointi 40 kwa mechi 15 ilizocheza.

Yalikuwa ni mabao ya Clement Mzize na Pacome Zouzoua yaliyoifanya kuondoka na ushindi wa tano ugenini katika mechi saba ilizocheza ikiwa mikoani.

Hakuna timu yoyote ya Ligi Kuu itakayofikisha pointi 40 itakapomaliza mechi zake 15 za mzunguko wa kwanza.

Yanga imeshinda mechi 12, sare moja, ikipoteza moja, mabao 36 ya kufunga na kuruhusu mabao manane kwenye wavu wake.

Mchezo huo uliochezwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, haukuwa rahisi kwa Yanga hasa kipindi cha pili, kwani ndicho ambacho Prisons ilikuja juu baada ya kufanya mabadiliko kadhaa.

Iliwachukua Yanga dakika saba tu kuandika bao la kwanza lililowekwa wavuni na Mzize, akiunganisha mpira wa krosi ya juu kutoka kwa Pacome.

Lilikuwa ni kosa la beki, Chilo Mkama, ambaye aliruka juu, lakini alishindwa kuuzuia mpira huo uliodondoka chini ya mguu wa mshambuliaji huyo akakwamisha wavuni likiwa ni bao lake la pili msimu huu kwenye Ligi Kuu.

Mzize nusura aipatie tena Yanga bao dakika ya 16, lakini haikuwa hivyo na ilipotimu dakika ya 19, Prisons ilifanya shambulizi lake la kwanza katika lango la Yanga.

Akiwa nje ya eneo la 18, Haji Mussa, aliachia shuti kali lililotoka nje kidogo ya lango.

Dakika ya 26, Samson Mbangula aliikosesha Prisons bao, aliporuka juu kuunganisha mpira wa faulo iliyopigwa na nahodha wa timu hiyo, Salum Kimenya, lakini kichwa alichopiga hakikulenga lango.

Pacome angeweza kufunga bao dakika ya 39, alipopenyezewa mpira ambao ulimkuta akitazamana na kipa Yona ana kwa ana, lakini akapiga fyongo.

Katika hali ya kushangaza, Maxi Nzengeli alikosa bao la wazi dakika ya 45, ambalo ilikuwa rahisi zaidi kupata kuliko kukosa akiwa yeye na lango tupu.

Mzize alitumbukiza krosi ambayo awali ilikoswa na Farid Mussa, mpira ukabaki umesimama ukisubiri yoyote yule atakayeukuta.

Maxi akiwa anatazamana na lango tupu, hatua moja tu kutoka golini, badala ya kuudokoa ili ujae wavuni, alipiga shuti kubwa, mpira ukanyanyuka juu na kwenda kugonga mwamba wa juu, ukarudi uwanjani.

Wakati kila mtu akiamini Yanga ingeenda mapumziko ikiwa na bao moja, Pacome alisawazisha makosa yake ya kukosa bao na mwenzake, alipopachika bao la pili.

Mfungaji aliuwahi mpira wa krosi iliyopigwa na Yao Kouassi, akabaki ana kwa ana na kipa Yona kabla ya kuukwamisha wavuni.

Linakuwa ni bao la nane kwa Pacome kwenye Ligi Kuu msimu huu, na ,asisti' ya sita kwa Kouassi akimfikia kinara wa pasi za mwisho, Kipre Junior wa Azam FC.

Kipindi cha pili hali ilibadilika, kwani

INAENDELEA UK. 23

## Simba waahidi furaha kubwa leo, waonywa

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI Kocha Daniel Cadena akisema hakuna kitu kingine kitakachofanyika leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza zaidi ya kuwarejeshea wanachama na mashabiki wa Simba furaha ambayo walishindwa kuipata Ijumaa iliyopita ilipotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Azam FC, wachezaji wa timu hiyo wameonywa.

Simba inashuka tena leo kwenye uwanja huo kucheza dhidi ya Geita Gold ikiwa ni mechi yake ya 14 ya Ligi Kuu Tanzania Bara kama ilivyo kwa wapinzani wao.

Cadena ambaye ni kocha wa magolikipa, alisema inabidi wafanye kazi kubwa ya kuwaandaa wachezaji vizuri licha ya kwanza hawana muda wa mapumziko wala kufanya mazoezi kutokana na ratiba kubana.

"Inabidi tufanye kazi kubwa kwa sababu hatuna muda wa kupumzika, wala wa kufanya mazoezi, lakini tupo tayari kwa mechi hii, tumewaandaa wachezaji wetu kwa ajili ya kutupa pointi tatu.

Katika mechi iliyopita tulicheza vizuri, ila haiwezekani wachezaji wote wakacheza kwa ubora ule ule wakati wanacheza michezo mfululizo, tunawaheshimu wapinzani wetu, lakini kwetu mechi hii ni muhimu kwa ajili ya kuwarudishia furaha wanachama na mashabiki wetu kwa kile kilichotokea kwenye uwanja huu," alisema Cadena ambaye alizungumza akikaimu ukocha msaidizi baada ya Selemani Matola kulimwa kadi nyekundu katika mechi dhidi ya Azam FC.

Beki wa kati ya timu hiyo, Hussein Kazi, kwa niaba ya wachezaji wenzake alisema pamoja na kwamba Geita Gold ni timu nzuri, lakini wamepania kuwapa furaha mashabiki wa Simba, pia ni mechi muhimu kwao kupata pointi tatu.

"Kwa niaba ya wachezaji wenzangu tumejiandaa vema kwa mechi hii ili kuwapa furaha wanachama na mashabiki wa Simba.

"Kila mchezo una presha yake, mechi dhidi ya Azam FC imepita na tuko kwa ajili ya kurudisha furaha ya mashabiki na morali yetu kama wachezaji, najua Geita Gold siyo timu mbaya, lakini sisi tunahitaji pointi tatu ili kutuweka kwenye njia sahihi ya kusonga mbele kutwaa ubingwa," alisema Kazi.

Kocha Msaidizi wa Geita Gold, Lucas Mlingwa, alisema wamepata bahati ya kuiangalia Simba inavyocheza, hivyo wamejiandaa kucheza kwa jinsi walivyoitazama.

"Tumetumia kipindi hiki cha mapumziko kuisoma na nadhani itakuwa ni faida kubwa kwetu kwani tumeshajua ni jinsi gani ya kuidhibiti," alisema.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >